# SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR

## AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

# HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/2027 ILIYOSOMWA KATIKA BARAZA LA WAWAKILISHI NA KAIMU WAZIRI WA NCHI, AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

**MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (MBM)**

**MEI, 2026**



**MHESHIMIWA HAMZA HASSAN JUMA (MBM)**

**KAIMU WAZIRI WA NCHI, AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS, ZANZIBAR.**

# YALIYOMO

YALIYOMO ........................................................ i
VIFUPISHO VYA MANENO ........................................ iv
A.UTANGULIZI ........................................................ 1
i. MIKAKATI YA UHIFADHI WA MAZINGIRA, UTOAJI WA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NA UKIMWI........................ 6
ii UHIFADHI WA MAZINGIRA, UTOAJI WA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NA MAAMBUKIZI MAPYA YA UKIMWI........... 6
B. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE ........................................................ 14
C. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA ........................................................ 15
i MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 .... 17
ii. MATUMIZI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 ........................................................ 18
iii.MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026. .................................. 19
D.UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA AMKR KWA JULAI 2025 – MACHI 2026. ........................................................ 31
PROGRAMU KUU P00201: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........................................................ 33

PROGRAMU KUU P00202: Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu ..........................................37
PROGRAMU KUU P00203: Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ......................46
PROGRAMU KUU P00204: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais ................................48
E.UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI,2025 – MACHI,2026 ..............................................49
PROGRAMU KUU P03401: Usimamizi wa Mazingira ..49
PROGRAMU KUU P03201: Udhibiti wa dawa za kulevya..........................................................54
Programu Kuu 03301: Uratibu Mwitiko wa Taifa Wa UKUMWI ..............................................................60
F.MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027..................................................................65
PROGRAMU KUU P01: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi ........................................................71
PROGRAMU KUU P04: Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ......................74
PROGRAMU KUU P03: Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais................................77
PROGRAMU KUU P02: Usimamizi wa Mazingira........78

PROGRAMU KUU P01: Udhibiti wa Dawa za Kulevya ........................................................... 80
PROGRAMU KUU P02: Uratibu wa Muitiko wa Taifa waUKIMWI ..................................................81
G.SHUKURANI..................................................................82
H.HITIMISHO ...................................................................85
I.VIAMBATANISHO ...........................................................86

## VIFUPISHO VYA MANENO

| | |
|---|---|
| AMKR | Afisi ya Mkamu wa Kwanza wa Rais |
| AYAHIZA | Asociation of Young People Against HIV and AIDS Zanzibar |
| BSAAT | Building Sustainable Anti corruption Action in Tanzania |
| CBID | Community Based Inclusive Development |
| CCM | Chama Cha Mapinduzi |
| CCTV | Closed Circuit Television |
| CFP | Community Forest Program |
| COFMA | Community Forest Management |
| COSTECH | Tanzania Commision for Science and Technology |
| DCEA | Drug Control and Enforcement Authority |
| DEA | Drug Enforcement Authority |
| DPP | Director of Public Prosecution |
| EBARR | Ecosystem Based Adaptation for Rural Resilience |
| ESA | European Space Agency |
| GST | Goods and Service Tax |
| ICT | Information and Communication Technology |
| ISD | International Institute for Suistainable Development |
| ILO | International Labour Organization |
| IPA | Institute of Public Administration |
| JKU | Jeshi la Kukuza Uchumi |
| KIST | Karume Institute of Science and Technology |

| | |
|---|---|
| KMKM | Kikosi maalum cha Kuzuia Magendo |
| KOICA | Korea Internation Co |
| KVZ | Kikosi cha Valantia Zanzibar |
| MoU | Memorandom of Understandings |
| NAP | National Adaptation Program |
| NCA | National Construction Authority |
| PBB | Program Based Budgeting |
| PBZ | People Bank of Zanzibar |
| PECCA | Pemba Chanel Conservation Areas |
| PGD | Post Graduate Diploma |
| PrEP | Pre – exposure Prophylaxis |
| SACCOS | Savings and Cradit Co operative Society |
| SAPPHIRE | Strategic Action Policy Program Hamonization and Instituional Reform |
| SDGs | Sectoral Development Goals |
| SHIJUWAZA | Shirikisho la Jumuia za Watu wenye Ulemavu |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar |
| TV | Television |
| TBC | Tanzania Broadcasting Company |
| TEHAMA | Taknologia ya Habari na Mawasiliano |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TZS | Tanzania Shilings |
| UNFCCC | United Nations Framework Convention on Climate change |
| UK | United Kingdom |
| UKIMWI | Ukosefu wa Kinga Mwilini |
| UMATI | Chama cha Uzazi na Malezi bora Tanzania |

| | |
|---|---|
| UNAIDS | United Nations Agency for International Development |
| UNDP | United Nation Development Program |
| UNEP | United Nation Environmental Program |
| UNODC | United Nations Office for Drugs and Crime |
| UPEPG | Uzi Island Planting mangroves and Environmental Protection Group |
| VVU | Virus Vya Ukimwi |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZAEEA | Zanzibar Economic Empowerment Agency |
| ZANGOC | Zanzibar NGOs Cluster for HIV/AID Prevention |
| LMSP | Local Marine Spatial Planning |
| ZJP | Zanzibar Joint Program |
| ZAYEDESA | Zanzibar Youth Education, Environmental Suport Association |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Company |
| ZBS | Zanzibar Bureau of Standard |
| ZCTV | Zanzibar Cable Television |
| ZDCEA | Zanzibar Drug Control and Enforcement Authority |
| ZGAMIS | Zanzibar Government Management Information System |
| ZYF | Zanzibar Youth Forum |

## HOTUBA YA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/2027

## A. UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika,** kwa ruhusa yako, naomba kutoa hoja kwa Baraza lako Tukufu likae kama Kamati ya Matumizi ili iweze kupokea, kujadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027.

2. **Mheshimiwa Spika**, Naomba nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu Mwingi wa Rehema kwa kutujaalia uzima na afya njema pamoja na kuibariki Nchi yetu kuendelea kuwa na amani, Umoja na Mshikamano. Ni dhahiri kwamba hali hiyo imezidi kuimarika chini ya uongozi mahiri wa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi ambae amekuwa akisisitiza umuhimu wa kudumisha amani kila anapokutana na viongozi mbalimbali wa Serikali, vyama, Dini mbalimbali na wananchi kwa ujumla. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaalie afya njema, busara na uwezo zaidi wa kuiongoza Zanzibar na kuleta maendeleo makubwa zaidi katika awamu hii ya pili ya uongozi wake.

3. **Mheshimiwa Spika,** Kwa namna ya kipekee naomba kutumia fursa hii kumpongeza kwa dhati Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi,

Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuchaguliwa tena kuwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi katika kipindi cha pili cha awamu ya nane ili kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar na kuacha alama ya maendeleo katika sekta mbalimbali nchini mwetu. Vilevile, nampongeza Mheshimiwa Rais wa Zanzibar pamoja na kusimamia vyema suala la amani nchini kabla, wakati na baada ya uchaguzi. Hii inatokana na jitihada mahsusi anazozichukua kiongozi wetu huyu mahiri katika kuendelea kusimamia na kusisitiza sana juu ya umuhimu wa kudumisha amani nchini.

4. **Mheshimiwa Spika,** vilevile, tunampongeza Mheshimiwa Rais kwa umahiri, ujasiri na ushupavu wake katika kuendeleza kudhibiti na kupambana na uingizaji, usafirishaji na matumizi ya dawa za kulevya nchini na kuimarisha nguvu kazi ya Taifa. Namuomba Mwenyezi Mungu amzidishie nguvu, afya njema, hekima na busara katika uongozi wake ili kufikia azma ya kuwaletea maendeleo bora wananchi wa Zanzibar pamoja na kusimamia vyema utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi 2025/2030, Mipango ya Maendeleo ya Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

5. **Mheshimiwa Spika,** shukrani za pekee ziende kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dk. Samia Suluhu Hassan kwa umahiri wake wa kuiongoza vyema Tanzania na kuimarisha mashirikiano makubwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dk.

Hussein Ali Mwinyi na hatimae kustawisha Muungano wetu kwa kuendelea kuimarisha amani na utulivu nchini. Aidha, jitihada zao za kukuza mashirikiano ya Kidiplomasia, Kubuni na kuendeleza miradi mipya ya maendeleo katika sekta mbali mbali zimesaidia pakubwa katika kuimarisha ustawi wa wananchi, ukuwaji wa demokrasia na uchumi wa Taifa letu.

6. **Mheshimiwa Spika,** Kwa dhati kabisa natumia nafasi hii kumpongeza Makamu wa Kwanza wa Rais Mstaafu, Mheshimiwa Othman Masoud Othman kwa kudumisha amani nchini na kuendelea kutekeleza jukumu lake la kumshauri vyema Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi pamoja na kusimamia vyema utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kipindi cha Julai hadi Oktoba 2025.

7. **Mheshimiwa Spika,** Pia nampongeza Makamu wa Pili wa Rais, Mheshimiwa Hemed Suleiman Abdulla, kwa kuteuliwa tena kuwa Makamu wa Pili wa Rais kwa kipindi cha 2025/2030 kwa ajili ya kuendelea kutekeleza majukumu ya Taifa akiwa ni msimamizi mkuu wa shughuli za Serikali. Namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie viongozi wetu hawa hekima, busara, siha njema, mashirikiano na mshikamano katika kuimarisha ustawi wa wananchi na maendeleo ya Taifa letu kwa ujumla.

8 **Mheshimiwa Spika,**Naomba kutumia nafasi hii kukupongeza wewe binafsi Mheshimiwa Zubeir Ali

Maulid kwa kuteuliwa tena kwa mara nyengine kuwa Spika wa Baraza la Wawakilishi Zanzibar. Aidha, mafanikio hayo yamepatikana kwa imani ya wajumbe na kwa namna unavyoliongoza Baraza la Wawakilishi ambalo limekuwa tulivu na kufanya wajumbe wa Baraza kuwa huru, kuchangia hoja na kutoa mawazo yao pasi na vikwazo kwa muda wote wa vikao vya Baraza. Vilevile, nampongeza Naibu Spika Mheshimiwa Mwanaasha Khamis Juma,Wenyeviti wa Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi kwa namna wanavyotoa hoja na michango iliyopelekea kuongeza ufanisi na uwajibikaji wa utendaji wa Taasisi na Idara mbalimbali na kuleta maendeleo ya nchini, namuomba Mwenyezi Mungu awazidishie uwezo wa utendaji, hekima na busara.

9. **Mheshimiwa Spika,** kwa niaba ya wafanyakazi wote wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais naomba kutumia nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Kusimamia Afisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa ya Baraza la Wawakilishi Mheshimiwa Machano Othman Said Mwakilishi wa wananchi jimbo la Mfenesini pamoja na Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati na Makatibu chini ya uongozi wake mahiri kwa namna unavyoendesha na kusimamia kwa umakini kazi za kamati kwa ustadi mzuri kabisa. Naomba nikiri kwamba ushirikiano wenu, michango na maelekezo mnayotupatia yamekuwa ni chachu kubwa ya kuleta mabadiliko chanya ya kiutendaji

yaliyopelekea kupatikana kwa mafanikio makubwa katika Afisi yetu.Vile vile, naomba niwashukuru kwa dhati wafanyakazi wote wa Baraza la Wawakilishi kwa Ushirikiano wanaotupatia katika kufanikisha majukumu ya Wizara yetu yetu.

10. **Mheshimiwa Spika,** Bila ya kusahau, naomba pia kuchukua nafasi hii kumshukuru kwa dhati Mheshimiwa Harusi Said Suleiman Waziri mstaafu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ushirikiano wake na uongozi wake mahiri katika kusimamia utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais katika kipindi cha kwanza awamu ya nane iliyoongozwa na Mheshimiwa Dk. Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Namuomba Mwenyezi Mungu amjaze kheri na baraka tele na ampe mafanikio na moyo wa kuendelea kulitumikia taifa kwa maendeleo ya nchi yetu.

11. **Mheshimiwa Spika,** nawashukuru wananchi wa jimbo la Shaurimoyo kwa kuendelea kuniamini pamoja na kuniunga mkono katika kazi zangu za uwaziri na Uwakilishi hadi leo. Naomba niwaahidi kuwa nitaendelea kuwatumikia kwa moyo wangu wote na kuwashirikisha katika maamuzi yatakayoleta maendeleo jimboni. Mwisho kabisa naomba niishukuru sana familia yangu kwa uvumilivu wao mkubwa na mashirikiano wanayonipa muda wote wa kutekeleza majukumu ya Kitaifa.

## B. MIKAKATI YA UHIFADHI WA MAZINGIRA NA UTOAJI WA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NA UKIMWI.

12 **Mheshimiwa Spika**, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina jukumu la usimamizi na uhifadhi wa Mazingira na kupunguza athari za mabadiliko ya tabianchi. Aidha, Afisi inaratibu mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya kwa kunusuru nguvu kazi ya Taifa, kusimamia upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu kwa kushiriki kikamilifu bila ya ubaguzi na kuimarisha upatikanaji wa kinga na tiba zenye ubora ili kumaliza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI ifikapo 2030. Dhamira hii imefikiwa na imetekelezwa kwa kuimarisha sekta zote zinazosimamia kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango Mkuu wa maendeleo wa Taifa (ZADEP 2021/2026), Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025/2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Kitaifa (SDGs), Mikataba ya kimataifa, Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo.

## C. KUIMARIKA KWA UHIFADHI WA MAZINGIRA, UTOAJI WA HUDUMA KWA WATU WENYE ULEMAVU NA MAPAMBANO DHIDI YA DAWA ZA KULEVYA NA MAAMBUKIZI MAPYA YA UKIMWI.

13 **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeimarisha ushirikiano wa pamoja katika kulinda

na uhifadhi endelevu wa mazingira ili kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, utoaji Huduma na haki sawa kwa watu wenye ulemavu, waathirika wa dawa za kulevya na Virusi vya UKIMWI na kuhakikisha kuwa jamii inakuwa ni sehemu ya ujenzi wa uchumi imara, shirikishi, endelevu na kuimarisha ustawi wa jamii nchini.

14. **Mheshimiwa Spika,** Uhifadhi wa mazingira ni jukumu la kila mwananchi kuhakikisha Nchi yetu inadumu, kwa kuzuia uchafuzi wa hewa, maji, na ardhi kupitia upandaji miti, utupaji taka sahihi, na kuepuka uharibifu wa misitu. Hatua hizi ni muhimu kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na kulinda uhai wa viumbe vyote. Hii ni muhimu kwa sababu mazingira safi na salama ndiyo msingi wa maisha na afya bora kwa manufaa ya sasa na vizazi vijavyo.

15. **Mheshimiwa Spika,** Rasimu ya awali ya ripoti ya Hali Halisi ya Mazingira ya miaka mitano (2021/2026) imeonesha kuongezeka kwa joto katika bahari na asidi ambayo imepelekea kufubaa kwa matumbawe, mmong'onyoko wa fukwe, kuongezeka kwa kina cha bahari, uingiaji wa maji ya baharí katika maeneo ya kilimo na makaazi, kupungua uzalishaji wa mwani na kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji taka. Vilevile, Afisi inaendelea na utayarishaji wa Mkakati mpya wa Mabadiliko ya Tabianchi.

16. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kuchukua juhudi za kutekeleza matakwa ya Mkataba wa

Kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi (UNFCCC) kwa kukamilisha mikakati ya Kitaifa, kikanda na kimataifa ikiwemo NDC 3.0, NAP pamoja kufanya tathmini ya maeneo 60 yanayoingia maji ya bahari na matayarisho ya michoro na gharama za ujenzi wa matuta, kuta za kuzuia maji ya Bahari katika maeneo ya Mtangani, Mtambwe, Ndagoni, Maisara na Bumbwini Mafufuni.

**17.** **Mheshimiwa Spika,** Jitihada mbalimbali zimeendelea kuchukuliwa katika kuimarisha usimamizi wa mazingira ikiwemo kudhibiti matumizi ya mifuko ya plastiki ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kilogramu 2,263 (Unguja 1,736.5 Kg, Pemba 526.5 Kg) zimekamatwa na kutozwa faini ya shilingi 9,100,000 (7,990,000 Unguja na 1,110,000 Pemba) ikilinganishwa na kilogramu 400 zilizokamatwa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Haya ni mafanikio makubwa yaliyopatikana katika kupunguza matumizi ya mifuko ya plastiki kupitia operesheni 54 katika maghala makubwa yanayohifadhi bidhaa mbali mbali Unguja na Pemba.

**18.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeimarisha Uhifadhi wa mazingira ambapo kwa mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya maeneo 139 yamekaguliwa kiwilaya ikilinganishwa na maeneo 185 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Aidha, ukaguzi umeonesha kwamba Wilaya ya Kati inaongoza ikifuatiwa na Chake chake, Magharibi B na Micheweni kwa kuwa ni maeneo yanayochimbwa rasilimali zisizorejesheka na maeneo

yanayokumbwa na changamoto za utapakaaji wa taka na maji machafu.Vile vile,Miongozo ya kimazingira iliyosaidia kupunguza kero, uchafuzi na uharibifu wa mazigira imetolewa na tathmini 101 za kimazingira (Unguja 68, Pemba 33) zilifanyika.

19. **Mheshimiwa Spika,** Haki sawa kwa watu wenye ulemavu ni haki za msingi za binadamu, zinazohakikisha usawa, utu, na ushiriki kikamilifu katika jamii bila ubaguzi. Haki hizi ni pamoja na kufikika kwa majengo, elimu, ajira, huduma za afya, na ulinzi dhidi ya unyanyasaji. Sheria na mikataba ya kimataifa na Kikanda inalazimisha kuondoa vizuizi vyote ili kuwawezesha kuishi kwa uhuru. Aidha, kwa mujibu wa sensa ya Watu na makaazi ya mwaka 2022 imeonesha ongezeko la Watu wenye Ulemavu kutoka asilimia 5.8 kwa mwaka 2012 hadi 11.4 kwa mwaka 2022 kwa wastani wa Watu wenye Ulemavu 195,772.

20. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea na utoajii wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu ambapo jumla vifaa saidizi 773 vikiwemo Motor Wheelchair 60, Sun screen lotion 377, kofia 236 na miwani 100 vyenye thamani ya shilingi 894,950,000 vimetolewa kwa mwaka 2025/2026 ikilinganishwa na vifaa saidizi 425 vyenye thamani ya shilingi Milioni 325,500,000 vilivyotolewa kwa mwaka wa fedha 2024/2025 .

21. **Mheshimiwa Spika,** Baraza la Watu wenye Ulemavu kwa kushirikiana na Wakala wa Uwezeshaji

Wananchi Kiuchumi limetoa unafuu wa masharti ya mikopo ya Watu wenye Ulemavu kupitia programu ya 4:4:2 ambapo kwa hivi sasa tumepunguza masharti yaliyokuwepo hapo awali yaliyosema kua Mikopo wapewe vikundi lakini kwa hivi sasa Sharti hilo limeondoka na inatoa fursa kwa mjasiriamali mmoja mmoja mwenye Ulemavu kuweza kupata mikopo hiyo. Jumla ya TZS 79,780,000 zimetolewa kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kwa Wajasiriamali wenye Ulemavu ikilinganishwa na TZS 43,200,000 zilizotolewa kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mafanikio haya yametokana na mabadiliko ya masharti na kutoa fursa ya mikopo kwa mtu mmoja mmoja, vikundi na watu wengi zaidi wenye Ulemavu. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya vikundi viwili (2) vinavyojumuisha wanufaika 37 (Wme 18 na Wke 19) na mtu mmoja mmoja 29 (Wme 21 na Wke 8) wamepatiwa mikopo hiyo.

22. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji dawa za kulevya nchini hatua iliyosaidia kunusuru kundi kubwa la vijana ambao wamekuwa waathirika wakubwa wa dawa hizo. Aidha, kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kilogramu 1,525.288 za dawa za kulevya zilizokamatwa na kutaifisha mali ikiwemo Nyumba, Magari, Mashamba na nyenginezo zenye thamani ya Tzs 1,135,800,000 ikilinganishwa na kilogramu 1449 za dawa za kulevya zilizokamatwa pamoja na kutaifisha mali zenye

thamani ya TZS 976,052,016 kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Mafanikio haya yamepatikana kutokana na ongezeko la operesheni, utoaji wa maamuzi ya kesi za uhalifu wa dawa na utaifishaji, mbinu za kiofisa katika ukamataji na utumiaji wa simu ya bure ya 119 na Mamlaka imeimarisha mashirikiano na wananchi pamoja na kuwajengea uwezo na mbinu maafisa doria katika kutoa taarifa za wahalifu wa dawa za kulevya.

23. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kutekeleza vielelezo vya dawa za kulevya vyenye uzito wa Kilogramu 781.39 ikiwemo Bangi kilogramu 562, Mirungi kilogramu 27.4, Kokeni kilogramu 0.08, Heroine kilogramu 6.4, Valium kilogramu 5.8, Codaine kilogramu 2.13, catemine kilogramu 0.03,morphine kilogramu 0.064, LSD kilogramu 0.06, LDM kilogramu 0.07,Panthetamine kilogram 0.01, Shisha kilogramu 0.95 na nyengine baada ya kukamilika kwa ushahidi Mahakamani ili kuinusuru jamii na matumizi ya dawa hizo.

24. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanikiwa kufungua kesi 48 (Unguja 40 na Pemba 8) ambapo watuhumiwa 53 (wanaume 45, wanawake 8) walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi, heroin na kokeni.

25. **Mheshimiwa Spika,** Waraibu 39 wanaendelea kupatiwa huduma za tiba na marekebisho ya tabia katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni

na familia 170 za vijana wanaopata huduma katika kituo hicho walipatiwa huduma ya tiba ya kifamilia (family therapy). Vilevile, waraibu 68 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ikijumuisha ufugaji ng'ombe, kilimo cha vitalu nyumba (green house), ufundi charahani na gereji ili kuwawezesha kujitegemea kiuchumi na kuepuka kurudia katika matumizi ya dawa za kulevya na waraibu wapya 143 walipokelewa kituoni hapo.

26. **Mheshimiwa Spika,** Mapambano dhidi ya maambukizi ya VVU/UKIMWI nchini Tanzania na duniani kote yanaendelea kwa kasi, huku yakilenga kufikia malengo ya "95-95-95" (asilimia 95 kujua hali zao, 95 kupata matibabu, na 95 kuwa na kiwango kisichopimika cha virusi) ifikapo 2026. Jitihada hizi zinajumuisha elimu kwa vijana, upatikanaji wa dawa za kufubaza virusi (ARV) na kinga (PrEP) kwa kushirikiana na Wizara ya Afya.

27. **Mheshimiwa Spika,** idadi ya watu waliopata maambukizi mapya kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ni 107 ikilinganishwa na watu 364 waliopata maambukizi kwa mwaka fedha 2024/2025. Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inaendelea na utekelezaji wa mkakati huo pamoja na kuongeza nguvu ya utoaji wa elimu kwa vijana katoka vyuo vya kati na vyuo vikuu, sekondari pamoja na makundi mbali mbali ili kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI hapa Zanzibar.

**28. Mheshimiwa Spika,** Afisi imetoa elimu ya VVU na UKIMWI kwa vijana 131,506 katika vyuo vikuu na imewafikia watu 21,593 kupitia vituo vya Tiba na huduma rafiki. Aidha, utoaji wa elimu kupitia mitandao ya kijamii ikiwemo Instagram, Facebook na TikTok iliwafikia watu 90,114 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikilinganishwa na watu 4,549 kwa mwaka 2024/2025. Afisi inaiomba Serikali kutenga bajeti ya kutosha ya kutoa Elimu kwa jamii kuhusu kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI kwani Washirika wa Maendeleo wameendelea kupunguza nguvu kwenye kusaidia mapambano dhidi ya maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI bila ya hivyo lile lengo letu la kufukia Asilimia 0 haitoweza kufikia hapo ifikapo mwaka 2030.

**29. Mheshimiwa Spika,** Huduma jumuishi za VVU ni mbinu ya kutoa matibabu ya VVU pamoja na huduma nyingine za afya (kama kifua kikuu, magonjwa yasiyoambukiza, na afya ya uzazi) katika eneo moja. Mbinu hii inalenga kurahisisha upatikanaji wa matibabu, kupunguza unyanyapaa, na kuboresha afya ya jumla ya wanaoishi na VVU. Aidha, kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Afisi imeimarisha utoaji wa huduma jumuishi za VVU na afya ya uzazi Katika kliniki za tiba ambapo, huduma za uzazi wa mpangilio zimetolewa kwa watu 2,589, maradhi ya kujamiiana 12,364, uchunguzi ya kansa ya shingo ya kizazi 1,509 na kondomu 338,044.

30. **Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, naomba sasa uniruhusu niweze kuwasilisha utekelezaji wa majukumu ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo:-

## C. VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YAKE

31. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilijipangia Vipaumbele yafuatayo: -

    1. Kutekeleza miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.
    2. Kutayarisha ripoti ya Hali Halisi ya Kimazingira kwa kipindi cha miaka mitano (5) 2020/2025.
    3. Kufanya Tathmini na Kuandaa Mpango Mkakati mpya wa Mabadiliko ya tabianchi
    4. Kuendeleza Mapambano dhidi ya dawa za Kulevya na kuimarisha utoaji wa huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia.
    5. Ujenzi wa Kituo cha wanawake cha Tiba na marekebisho ya Tabia Kangagani Pemba pamoja na kuendeleza miradi ya ujasiriamali kwa waraibu.
    6. Kukuza uwezeshaji, ujumuishwaji na upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo.
    7. Kutayarisha na kutekeleza Miongozo 2 na Mikakati 2 ya masuala Watu wenye Ulemavu.

## A. UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA MSINGI YA WIZARA

**32. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilijipangia majukumu yafuatayo:-

i. Kutekeleza miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya kijani.
ii. Kutayarisha ripoti ya Tathmini ya Kimazingira kwa kipindi cha miaka mitano (5) 2020/2025.
iii. Kufanya Tathmini na Kuandaa Mpango Mkakati mpya wa Mazingira
iv. Kuendeleza Mapambano dhidi ya dawa za Kulevya na kuimarisha utoaji wa huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia.
v. Ujenzi wa Kituo cha wanawake cha Tiba na marekebisho ya Tabia Kangagani Pemba pamoja na kuendeleza miradi ya ujasiriamali kwa waraibu.
vi. Kukuza uwezeshaji, ujumuishwaji na upatikanaji wa haki na fursa kwa Watu wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo.
vii. Kutayarisha na kutekeleza Miongozo 2 na Mikakati 2 ya masuala Watu wenye Ulemavu.
viii. Kuwatambua watu wenye ulemavu nchini kwa kuwasajili katika mfumo wa Kidigitali wa kuhifadhia taarifa za watu wenye ulemavu.
ix. Kuratibu utekelezaji wa mkakati wa IV wa UKIMWI ili kudhibiti maambukizo mapya ya UKIMWI kwa vijana, makundi maalumu na jamii kwa ujumla

x. Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano na Utetezi wa UKIMWI kwa vijana kwa kuanzisha Mkakati wa Nne waTaifa wa UKIMWI, miongozo ya kitaifa na kisheria ya UKIMWI.

xi. Kuratibu na kutekeleza shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kuimarisha mashirikiano ya Kimataifa, Kikanda na kisekta baina ya SMZ, SMT na wadau.

**33. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais iliendelea kusimamia miradi mitano (5) ya maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
ii. Mradi wa kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za pwani ya Zanzibar unaofadhiliwa na Adaptation Fund;
iii. Mradi wa usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Washirika;
iv. Mradi wa ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar; na
v. Mradi wa Kuimarisha mifumo ya Kitaifa na kuziwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi (SCALE) unaofadhiliwa na Benki ya Dunia ambao unatarajiwa kutekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano 2025/2030 ambapo jumla ya Dola za Kimarekani 110,0000,000 zimetengwa

kwa Wilaya 56 za Tanzania (45 Tanzania Bara na 11 Zanzibar).

**34.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imeendeleza mashirikiano na Taasisi mbali mbali zikiwemo UNEP, UNDP, IOC, Global Network, Taasisi ya Uongozi Tanzania na Asasi za kiraia (NGO) ya CAN-TZ katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazingira na kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

i. Mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa jamii ya pwani katika maeneo ya Bumbwini Mafufuni-Unguja, Kiongwe kidogo na Tovuni kwa upande wa Pemba
ii. Mradi wa uimarishaji na mfumo wa maji machafu katika Manispaa ya Chake Chake -Pemba
iii. Mradi wa kuimarisha jamii kwa kuzingatia ikolojia na shughuli za kujipatia kipato kwa wavuvi wadogo wadogo na usimamzi wa eneo la hifadhi la mkondo wa PECCA
iv. Tathmini ya kina ya maeneo mbali mbali yaliyoathirika na uingiaji wa maji ya bahari katika kisiwa cha Pemba

## i.MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**35.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, ilipangiwa kukusanya jumla ya Shilingi Milioni 700,801,000 kupitia vyanzo vya mapato ambavyo ni ada ya uhifadhi wa mazingira na ada ya ukaguzi wa mazingira. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi

Machi, 2026, jumla ya **Tsh Milioni 529,100,000** zilipangwa kukusanywa ambapo jumla ya **Tsh Milioni 389,440,000** sawa na **asilimia 74** zimekusanywa. ***Kiambatanisho nambari 1 kinahusika.***

## ii. MATUMIZI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA KIPINDI CHA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**36. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 Afisi ya Makamu wa kwanza wa Rais iliidhinishiwa matumizi ya **TZS. 27,182,108,000** (Mishahara **TZS. 6,941,400,000**, Matumizi mengineyo **TZS.5,883,411,295**, Miradi ya Maendeleo **TZS.12,413,196,705** na Ruzuku ya **TZS.1,944,100,000** katika hizo **TZS .1,294,000,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 650,100,000** kwa ajili ya mishahara). Pia Afisi imeidhinishiwa jumla ya **TZS. 12,413,196, 705** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ( **TZS. 10,000,000,000** kutoka SMZ na **TZS. 2,413,196,705** kutoka kwa washirika wa maendeleo).

**Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ilipangiwa matumizi ya **TZS.23,194,698,693** katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo **TZS. 5,340,651,284** zilitengwa kwa ajili ya mishahara, na **TZS .4,563,488,614** zilitengwa kwa ajili ya matumizi mengineyo, Ruzuku ni **TZS. 1,563,990,000** (**TZS.490,240,847** kwa ajili ya

mishahara na **TZS. 1,073,749,153** kwa ajili ya matumizi mengineyo) na Miradi ya Maendeleo **TZS. 11,726,558,795** (**TZS. 9,500,000,000** kutoka SMZ na **TZS. 2,226,558,795** kutoka kwa washirika wa maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **TZS. 9,283,101,143** sawa na asilimia **40** zilipatikana kwa kazi za kawaida ambapo **TZS. 5,155,577,964** sawa na asilimia **97** ni kwa mishahara na **TZS. 2,048,261,120** sawa na asilimia **45** ni kwa matumizi mengineyo na **TZS. 761,939,244** ni kwa ajili ya matumizi ya Ruzuku sawa na asilimia **49**.

**37. Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa kazi za maendeleo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya **TZS. 1,317,322,815** sawa na asilimia 11 zilipatikana kutoka kwa washirika wa maendeleo. ***Kiambatanisho nambari 2 kinahusika.***

## iii. MAFANIKIO NA CHANGAMOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026.

### a. Mafanikio

**38. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imepata mafanikio makubwa katika kuleta maendeleo ya kisekta, upatikanaji wa haki, fursa na ustawi wa makundi mbali mbali nchini kama ifuatavyo:-

i. Afisi imekamilisha utekelezaji wa mradi wa Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kutumia Mfumo wa Ikolojia Vijijini ambao ulitekelezwa katika Shehia

tatu za Matemwe zikiwemo Mbuyutende, Jugakuu na Kijini ambapo kituo cha ushoni na upakasaji wa ukili, usarifu wa sabuni na manukato na kituo cha mafunzo cha kilimo na mifugo vilikabidhiwa rasmi Wilaya ya Kaskazini A kwa lengo la kuendelea na shughuli za kujipatia kipato kwa jamii husika.

**39. Mheshimiwa Spika,** Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Makamu wa Rais (SJMT), Wizara ya Uchumi wa Buluu na Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo imepata miradi miwili na Programu moja ambayo ni Mradi Jumuishi wa Kuimarisha Uhimilivu wa Jamii na Mifumo Ikolojia ya Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi kwenye misitu ya miombo kwa Tanzania Bara na maeneo kame ya Zanzibar, Mradi Shirikishi wa Kuhimili mifumo Ikolojia ya bahari na Ukanda wa Pwani pamoja na shughuli za kujipatia kipato katika eneo la Kusini Mashariki Pemba na Programu Jumuishi ya Kukijanisha Tanzania. Vile vile, Afisi kwa kushirikiana na UNEP Tanzania inatekeleza Mradi Jumuishi wa Kuhimili Mabadiliko ya Tabianchi.

v. Afisi imesaini hati ya makubaliano na kampuni ya TULIVE kutoka Namibia yenye lengo la kushirikiana katika kuibua fursa zilizopo Zanzibar za biashara ya Kaboni kwenye maeneo ya usafirishaji wa njia ya anga na bahari ili kupunguza gesi joto;

vi. Afisi kwa kushirikiana na Afisi ya Rais Muungano na Mazingira imefanikisha vizuri mkutano wa kwanza wa kimataifa kwa kundi la wataalamu wa Afrika

(AGN) kuhusu mabadiliko ya Tabianchi uliofanyika Zanzibar ambapo Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alikuwa Mwenyekiti wa kundi hilo. Aidha, Afisi imeshiriki kikao cha mashirikiano baina ya SMZ na SJMT katika sekta ya mazingira kwa lengo la kubadilishana uzoefu na kupelekea kutayarisha hati za makubaliano baina ya ZEMA na NEMC.

vii. Mkutano wa mashirikiano baina ya ZDCEA na DCEA na Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu na Qatar charity Organization umefanyika kwa lengo la kuimarisha mashirikiano na kubadilishana uzoefu na kusaidiana katika kutatuwa changamoto zinazoikabili sekta husika;

viii. Afisi kwa kushirikiana na Wizara ya Ardhi na Maaendeleo ya Makaazi imewapatia ardhi yenye ukubwa wa mita za mraba 9,756.11 iliyopo kibele kwa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu, mita za mraba 1, 273.53 iliyopo chuini kwa shirikisho za jumuiya za watu wenye ulemavu Zanzibar (SHIJUWAZA) na mita za mraba 1,270.81 iliyopo chuini kwa jumuiya ya wanawake wenye ulemavu Zanzibar (JUWAUZA) kwa lengo la ujenzi wa afisi kituo cha marekebisho kwa watu wenye ulemavu na huduma na makaazi kwa maendeleo jumuishi. Aidha, Afisi kwa kushirikiana na ZBA ipo katika hatuwa za mwisho za mapitio ya michoro na gharama za ujenzi wa afisi za SHIJUWAZA;

ix. Serikali imeimarisha utowaji wa haki na ushirikishaji wa Watu wenye Ulemavu katika nafasi za maamuzi tisa (9) wakiwemo Wawakilishi wawili (2) Wabunge wawili (2), Diwani mmoja (1), Waziri mmoja (1), Katibu Mkuu mmoja (1) na Wakurugenzi wawili (2) jambo ambalo halijawahi kutokea huko miaka ya nyuma, tunampongeza Rais wetu Dk Hussein Ali Mwinyi kwa kuwajali watu wenye Ulemavu katika Serikali yake ya awamu ya nane.

x. Afisi imetayarisha rasimu ya muongozo wa mfuko wa maendeleo wa watu wenye ulemavu na rasimu ya mipango mkakakti wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu kwa kipindi cha miaka mitano (2025/2030)

xi. Afisi imekamilisha maboresho ya mfumo wa kuhifadhia tarifa za watu wenye ulemavu ujulikanao kwa jina la JUMUISHI Management Information system ambao umeunganishwa vitambulisho vya Zanzibar na vizazi na vifo jambo ambalo litasaidia sana upatikanaji wa huduma kwa watu wenye ulemavu Zanzibar.

xii. Afisi kupitia Baraza imefanya ukaguzi kwa majengo 10 ya umma katika Wizara tano (5) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambapo asilimia kubwa ya majengo hayo yamezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu na pia kutoa Miongozo kwa yale ambayo hayakuzingatia mahitaji hayo.

xiii. Afisi kupitia Mamlaka ya Udhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya hivi karibuni imefanikiwa kugundua mbinu mpya inayotumiwa kuingiza na kutumia njia mbadala wa matumizi hatari ya dawa za kulevya na kufanikiwa kumkamkamata Raia mmoja wa Romania na wenzake kwa kuingiza dawa ya kulevya na kuyachanganya kwenye vyakula vya kawaida ikiwemo Pipi, Korosho na Biskuti ambapo huchanganywa na dawa za kulevya na kuyauza kwenye Supermarkets na Maduka mengineyo ya kawaida ambapo huwauzia hata raia wa kawaida wakiwemo watoto ambao baadae watakujakua waraibu kwa kuzoea kutumia dawa za kulevya bila ya kukusudia. Mamlaka imeyafunga maduka hayo pamoja na ghala moja liliopo Mpendae ambalo ndilo linalotumiwa kwa kuchanganyia dawa hizo kwenye vyakula vilivyotajwa hapo awali na kesi ya watuhumiwa hao inaendelea.

xiv. Afisi imefanikiwa kufungua kesi 48 (Unguja 40 na Pemba 8) ambapo watuhumiwa 53 (wanaume 45, wanawake 8) walikamatwa kwa tuhuma za kujihusisha na usafirishaji na usambazaji wa dawa za kulevya aina ya bangi, mirungi, heroin na kokeni.

xv. Afisi imeanzisha Kituo cha mawasiliano ya dharura kwa kurahisisha utoaji wa taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu uhalifu wa dawa za kulevya. Lengo ni kuiwezesha jamii kuripoti matukio au viashiria vya uhalifu wa dawa za kulevya wakati wowote kwa haraka na usiri kwa kutumia namba ya bure 119.

Hadi sasa jumla ya simu 122 zimepokelewa kuripoti taarifa mbalimbali za uhalifu wa dawa za kulevya ambapo taarifa 52 sawa na asilimia 43 zimefanyiwa kazi na kufanikisha kuwakamata wahalifu na taarifa 70 sawa na asilimia 57 zinaendelea na uchunguzi. Mafanikio haya yote yaliyopatikana yametokana na mashirikiano ya Wananchi ambao wamechoka na vitendo vya wanaofanya biashara ya dawa za kulevya kwa kutupatia taarifa kupitia njia ya simu na kuzifanyia kazi jambo ambalo limetusaidia sana kupata taarifa za uhakika kwa wanaofanya biashara hii haram, tunatoa wito kwa wananchi wengine kutupatia taarifa za Wahalifu hao na tunawaahidi tutawalinda na wala hatutowataja ili kulinda Uhuru wao wa kuishi kwa Amani amani bila ya kupata vitisho vinavyotokana na Maharamia hao wenye kuhusika na biashara hiyo ya dawa za kulevya.

xvi. Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imekamilisha hatua za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa kituo cha wanawake cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kangagani- Pemba. Hivi sasa tunasubiri ruhusa ya Serikali tuanze ujenzi wa Kituo hicho kwani Unguja kipo lakini kwa upande wa Pemba hakipo jambo ambalo pia linaleta usumbufu kwa waathirika wa dawa za kulevya kukosa huduma muhimu za kuwapatia Tiba na huduma nyingine kwa upande wa Pemba. Tunaomba Serikali kutupatia pesa ili tuweze kutekeleza mradi huo ndani ya mwaka huu wa Fedha.

xvii. Afisi imefanikisha maadhimisho ya siku ya UKIMWI duniani tarehe 1 Disemba 2025 na siku ya Watu wenye Ulemavu duniani tarehe 3 Disemba 2025. Kiambatanisho Nambari 3 Kinahusika

## 6.0 CHANGAMOTO ZILIZOJITOKEZA WAKATI WA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS

40. **Mheshimiwa Spika,** Pamoja na mafanikio yaliyopatikana, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakabiiliwa na changamoto zifuatazo: -

i. Uhaba wa wataalamu wa mazingira, mabadiliko ya tabianchi pamoja na biashara ya kaboni;

ii. Kuongezeka kwa athari za mabadiliko ya tabianchi ikijumuisha uingiaji wa maji ya chumvi katika maeneo ya makaazi na mashamba pamoja na mmong'onyoko wa ardhi katika maeneo ya fukwe na ongezeko la joto katika baharí ambapo zaidi ya maeneo 148 yameathiriwa na mabadiliko ya tabianchi. Aidha, maeneo ya Mtangani, Mtambwe, Maisara, Fumba, Nungwi, Pwani Mchangani, Bumbwini, Tumbatu, Gando bonde la Mpenja, haya ni miongoni mwa maeneo yaliyoathirika sana na yanahitaji hatua za haraka.

iii. Uharibifu wa mazingira unaosababishwa na ongezeko la Uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka;

iv. Ongezeko la uzalishaji wa taka ambapo kwa siku umefikia tani 654 na uwezo wa manispaa zetu si zaidi ya asilimia 50 jambo ambalo linaendelea kuharibu mandhari ya nchi yetu;
v. Ufinyu wa nafasi za Afisi unaopelekea uhaba wa nafasi za kufanyia kazi katika sekta ya mazingira;
vi. Jamii kuwa na muhali wa kutoa taarifa za uhalifu wa dawa za kulevya katika maeneo yao;
vii. Kuendelea kuwanyanyapaa Watu wenye Ulemavu na waathirika wa UKIMWI;
viii. Kuongezeka kwa ajali za barabarani na maradhi yanayopelekea kupata ulemavu;
ix. Kuwepo kwa watu wenye kuwatumia Watu wenye Ulemavu katika shughuli za ombaomba;
x. Ugumu wa kutoa elimu ya afya ya uzazi na VVU kwa vijana waliopo Skuli unaotokana na vikwazo vya mtaala wa Skuli za Zanzibar;
xi. Wadau wa maendeleo kupunguza mchango wao katika mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI;
xii. Ufinyu wa bajeti ambao hauendani na mahitaji ya utekelezaji wa majukumu ya afisi ambao pia unapelekea usumbufu wa vifaa na vyombo vya usafiri.

## 6.1 HATUA ZA UTATUZI WA CHANGAMOTO

**41. Mheshimiwa Spika,** Pamoja na changamoto zilizojitokeza Afisi imechukua hatua zifuatazo:-

i. Afisi imefanya mazingatio ya wataalamu hao katika mpango wa ajira (Norminal roll) ya mwaka

2026/2027 ambapo hadi sasa jumla ya nafasi 6 mpya za ajira zimependekezwa. Vilevile, tumepata uhamisho wa wataalamu wawili kutoka wizara ya elimu pamoja na kuimarisha mashirikiano na Taasisi za mazingira ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania;

ii. Afisi imeendelea na jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi zikijumuisha ujenzi wa kuta na matuta kwa ajili ya kuzuia maji ya baharí kuingia katika makaazi pamoja na mashamba ambapo kwa mwaka wa fedha wa 2025/2026 jumla ya TZS.4,500,000,000 zimetengwa kwa ajili ya kuhami maeneo ya Mtangani, Gando, Maisara, Mtambwe na Bumbwini. Afisi ipo katika matayarisho ya ujenzi wa hodhi la kuvunia maji ya mvua kwa shughuli za kilimo huko Bumbwini, upandaji wa miti aina mbali mbali ikiwemo mikoko, uwezeshaji wananchi katika ufugaji wa nyuki kwa lengo la kuinua kipato cha jamii na kuhifadhi mazingira. Vile vile, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kushirikiana na Afisi ya Makamu wa Rais Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imetayarisha rasimu ya mchango wa Taifa wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi (National determined contribution) wa miaka Mitano 2026/2030.

iii. Afisi imeimarisha operesheni na doria katika kudhibiti uchimbaji holela wa maliasili zisizorejesheka kwa kuhusisha vikosi vya SMZ na uongozi wa halmashauri. Aidha, afisi imeitisha kikao cha wadau

na kutoa mapendekezo juu ya hatua muafaka za kuchukuliwa katika kudhibiti na kuzuia uchimbaji wa rasilimali zisizorejesheka ikiwemo mapitio ya faini, uundaji wa vikundi vya ulinzi shirikishi katika shehia pamoja na uundaji wa kamati ya Mawaziri wanaoshughulikia sekta husika.

iv. Afisi imefanya vikao na wadau mbali mbali wakiwemo Taasisi, Sekta binafsi, wafanya biashara, Halmashauri na Manispaa katika udhibiti na uhifadhi wa taka ngumu na maji machafu. Aidha, afisi imeandaa rasimu ya kanuni ya usimamizi wa taka zinazotokana na bidhaa chakavu za umeme na electroniki (e-west) ambayo ipo katika hatua ya kuwasilishwa Serikalini, na muongozo wa usimamizi wa maji machafu ambao umeshawasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu kwa kupata maoni. Vile vile, Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kushirikiana na Kamisheni ya Utalii wameanzisha Programu ya uchambuzi wa taka ngumu katika mahoteli ya kitalii kwa Mkoa wa Kusini na Kaskazini Unguja.

v. Afisi imepatiwa kiwanja Maruhubi kwa ajili ya ujenzi wa jengo la afisi za ZEMA na tayari imeandaa michoro na gharama za ujenzi na kuwasilisha maombi ya fedha Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya ujenzi wa jengo hilo;

vi. Afisi bado inaendelea kuhamasisha jamii na kutoa elimu kupitia mikutano ya ana kwa ana katika

wilaya na shehia, vyombo vya habari pamoja na makundi na rika mbalimbali ili kueleza madhara yatokanayo na matumizi ya dawa za kulevya kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Aidha, afisi imeanzisha kituo cha kutolea tarifa za uhalifu wa dawa za kulevya (calling centre 119) ili kurahisha upatikanaji wa taarifa kutoka kwa jamii;

vii. Afisi inaendelea na utowaji wa elimu kupitia vyombo vya habari, vipeperushi, mitandao ya kijamii na midahalo inayohusisha makundi ya rika mbali mbali juu ya utowaji wa haki na fursa sawa kwa watu wenye ulemavu na maambukizi ya VVU na UKIMWI kwa jamii hususan vijana pamoja na kuhamasisha watoa maamuzi na watoa huduma pamoja na walezi na jamii kwa ujumla katika kuondosha tabia ya unyanyapa kwa watu wenye ulemavu na watu waishio na virusi vya UKIMWI.

viii. Afisi inaendelea kutoa elimu kwa jamii na kuzishajihisha mamlaka husika kuchukuwa hatua stahiki za kuepusha matukio na madhara yanayopelekea ulemavu,

ix. Afisi inaendelea kushajihisha watu wenye ulemavu kwa kuwatambua, kuwaunganisha katika vikundi, kuwapatia elimu ya ujasiriamali na kuwawezesha kiuchumi kwa kuwapatia mikopo ya 4:4:2, mashine, vifaa vya uzalishaji mali na kuwaunganisha na masoko ili waepukane na tabia ya kuombaomba.

x. Afisi imeendelea kuhamasisha na kuelimisha watoa maamuzi na kuwasilisha takwimu ili kubadili mtazamo juu ya vijana na hatari wanazokabiliana nazo juu ya maambukizi ya VVU na mimba za umri mdogo ili kuunga mkono juhudi za kuwafikishia elimu kulingana na umri na makuzi yao.

xi. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imeongeza bajeti ya ununuzi wa Kondomu, vitendanishi, vifaa tiba na kuhakikisha upatikanaji wa ARVs hapa nchini wakati wote ambapo kazi hii ipo chini ya Bohari ya dawa katika Wizara ya Afya kwa lengo la kupunguza utegemezi wa washirika wa maendeleo katika Programu za UKIMWI.

xii. Afisi inaendelea kuhamasisha wadau wakiwemo Mashirika ya kimataifa, Asasi za kiraia pamoja na vyanzo mbali mbali vya ndani katika upatikanaji wa rasilimali fedha kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Jumla ya maandiko 7 ya miradi yamewasilishwa Tume ya Mipango na Mashirika mbalimbali wakimwemo World Bank, ICUM, African development Bank, Uropean Union, Qatar charity, Tume ya Mipango, Ubalozi wa Brazili, UAE na Saudi Arabia.

## B. UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA NA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA AMKR KWA JULAI 2025 – MACHI 2026.

42. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imetekeleza majukumu yake kupitia Mfumo wa Bajeti unaotumia Programu (PBB) kupitia mafungu manne ya bajeti ambayo ni fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais), fungu B04 (Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira), C04 (Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya) na C05 (Tume ya UKIMWI).

43. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ilitekeleza majukumu yake kupitia programu zake kuu saba (7) ambazo ni:-

    i. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi;
    ii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu;
    iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
    iv. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya;
    v. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI;
    vi. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais; na
    vii. Programu ya Usimamizi wa Mazingira.

## MATUMIZI YA FUNGU B01 KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026 (AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS)

44. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kupitia fungu B01 (Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais) ilikadiriwa kutumia jumla ya TZS.12,977,235,876. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Afisi ilikadiriwa kutumia TZS. 11,192,825,909 Kati ya fedha hizo TZS. 2,121,224,999 ni kwa ajili ya Mishahara; TZS. 1,758,302,364 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, TZS. 1,563,990,000 ni kwa ajili ya Ruzuku; TZS. 5,749,308,545 ni kwa kutekeleza Miradi ya Maendeleo ambapo TZS.4,500,000,000 kutoka Serikalini na TZS. 1,249,308,545 kutoka kwa Washirika maendeleo.

45. **Mheshimiwa Spika,** Kwa kipindi Julai hadi Machi 2026 Kupitia fungu B01,imepangiwa kutumia TZS.11,192,825,909 ambapo TZS. 6,468,031,503 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; TZS. 1,563,990,000 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu, TZS. 931,377,131 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais na TZS. 2,229,427,275 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na TZS 820,227,088 kwa programu ya uratibu na utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba. ***Kiambatanisho nambari 2 kinafafanua***

46. **Mheshimiwa Spika,** Hadi kufikia Machi 2026, fedha zote zilizoingizwa ni TZS. 4,373,547,150 ambayo ni sawa na asilimia 39 ya utekelezaji. Kati ya fedha hizo TZS. 2,068,812,628 ni kwa ajili ya Mishahara ambayo sawa na asilimia 98; TZS. 662,664,579 ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo sawa na asilimia 38; TZS.761,939,243.5 ziliingizwa kwa matumizi ya Ruzuku ambayo sawa na asilimia 49 na TZS. 880,130,700 ni kutoka kwa wadau wa maendeleo sawa na asilimia 39.

47. **Mheshimiwa Spika,** fedha zilizopatikana kupitia programu za fungu 002, TZS. 1,230,256,115.5 ni kwa ajili ya kutekeleza Programu ya Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; TZS. 761,939,243 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu ya Watu wenye Ulemavu, TZS. 580,206,303.5 kwa ajili ya kutekeleza Programu Kuu Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais na TZS. 1,801,145,287 kwa ajili ya programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na TZS. 880,130,700 na TZS.713,927,279 kwa ajili ya Programu utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba sawa na asilimia 39 zilipatikana kwa ajili ya kazi za maendeleo.

## Programu Kuu P00201: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi

Matokeo ya Muda Mrefu: Kuwa na mazingira endelevu pamoja na kupungua kwa athari za mabadiliko ya tabianchi

**48. Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ilipangiwa kiasi cha TZS. 6,468,031,503. Hadi kufikia Machi 2026, imepatiwa matumizi ya TZS.1,230,256,115.5 (Matumizi ya Kawaida 66,608,353 na Mishahara 283,517,062 na maendeleo 880,130,700) sawa na asilimia 19 ya utekelezaji programu zake ndogo.

**49. Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa kipindi cha Julai – Machi kwa mwaka wa fedha 2025/2026, imetekeleza yafuatayo: -

a) Afisi imekuza uelewa wa biashara ya kaboni kupitia wadau wakiwemo Taasisi za Serikali, Asasi za kiraia pamoja na kamati za hifadhi ya misitu ya jamii (COFMA) juu ya uwepo wa fursa ya biashara ya kaboni. Aidha, zoezi la mapitio ya mikataba kwa ajili ya uwekezaji wa biashara ya kaboni yamefanyika ambapo jumla ya Kampuni 3 ambazo ni Sazani Associate, Terra Global na Tulive Private Equity LTD ya Namibia.

b) Afisi kupitia maonesho ya kitaifa ya Kilimo na biashara yaliyofanyika katika maeneo ya maonesho ya Dole na Nyamanzi, Mkoa wa Mjini Magharib Unguja imewafikia wananchi 574 waliotembelea banda la Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na kupata elimu, miongozo na ushauri juu ya uhifadhi na utunzaji wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi;

c) Afisi imetayarisha na kurusha vipindi viwili vya redio kupitia ZBC Redio na Spice FM juu ya mada ya taka ni mtaji.

d) Afisi imetayarisha kitini cha kilimo kinachostahamili mabadiliko ya tabianchi kilicholenga kutumika katika maeneo yanayoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya Zanzibar;

e) Afisi imetayarisha michoro pamoja na gharama za ujenzi kupitia mradi wa mazingira na utalii. Mradi huo utajumuisha ujenzi wa daraja la mbao (board walk), katika eneo la Mikoko, Tibirinzi, maeneo ya malazi (Cottage) pamoja na huduma nyengine za kukuza utalii wa kimazingira katika eneo hilo, ukumbi wa mkutano, vyumba vya wageni, maeneo ya kuogelea, maegesho ya magari katika eneo la Mikoko Tibirinzi Chakechake Pemba. Vilevile, kwa kushirikiana na Wakala wa Majengo Zanzibar (ZBA) michoro ya kuta, matuta na gharama za ujenzi katika maeneo ya Mtangani, maisara, ndagoni na bumbwini.

f) Matayarisho ya ujenzi wa hodhi la kuvunia maji ya mvua lenye uwezo wa kuhifadhi mita za ujazo 1,800 huko Bumbwini Mafufuni yamekamilika na ujenzi utaanza mara baada ya kupatikana kwa mkandarasi wa ujenzi.

g) Afisi ilitoa mafunzo na kushiriki katika mikutano na warsha mbalimbali nchini yenye malengo tofauti ikiwemo biashara ya kaboni, mpango wa matumizi

ya bahari na bioanuai. Vilevile, Afisi ilipata fursa ya kushiriki katika mikutano mbali mbali ya kikanda na kimataifa ya Nchi Wanachana wa Mikataba ya Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Mkutano wa kwanza wa Kamati ya Uongozi ya Mabadiliko ya tabianchi (Streering Committe meeting) uliolenga kupeana taarifa juu ya shughuli pamoja na miradi ambayo inatekelezwa na Idara ya Mazingira.

h) Afisi inatekeleza programu ya kuziwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi (SCALE PROGRAMME) wenye lengo la kuzijengea uwezo Taasisi za Kitaifa na katika ngazi ya Jamii, kufanya uwekezaji wa miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabianchi ndani ya jamii.

i) Afisi inatekeleza programu jumuishi ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira Zanzibar (ZJP) kwa kushirikiana na washirika mbalimbali wa Maendeleo. Kupitia programu hii ziara ya kimafunzo ya ufugaji nyuki na usimamizi wa mikoko imefanyika katika Wilaya ya Kilwa ambapo jumla ya washiriki 30 wakiwemo wanajamii 20 na wataalamu 10 wamepatiwa mafunzo hayo. Vilevile, tathmini ya hali ya ufugaji nyuki katika shehia za tatu Bumbwini (Makoba, Mafufuni na Kiongwe Kidogo) imefanyika. Aidha, Kitini cha kufundishia masuala ya ufugaji nyuki na usimamizi wa mikoko kimeandaliwa ambapo kwa kutumia kitini hicho,

mafunzo ya siku kumi (10) yamefanyika. Jumla ya wanajamii 70 wamepatiwa mafunzo hayo.

j) Afisi imefanya tathmini ya kina ya athari ya mabadiliko ya tabianchi katika kisiwa cha Pemba kwa kushirikiana na Taasisi ya International Institute for Suistainable development na NAP Global Network ya Canada.

k) Mafunzo ya ufugaji Kaa na Kamba yametolewa kwa vikundi vitatu vya Tibirinzi na Kamati ya Uhifadhi wa Misitu ya Tibirinzi pamoja na kufanya ziara ya kujifunza kwa vitendo ufugaji huo Sizini Pemba. Jumla ya watu 46 walipatiwa mafunzo hayo.

**50. Mheshimiwa Spika,** Huduma mbalimbali za utawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo kulipa stahiki za likizo kwa watumishi watatu (3), malipo ya muda wa ziada wa kazi kwa watumishi watano (5), mtumishi mmoja amelipwa ubani wa ufiwa na mtumishi 1 amelipiwa ada ya mafunzo ya muda mrefu ya Shahada ya kwanza katika fani ya Manunuzi. Vilevile, Huduma mbalimbali za utawala zimetolewa zikiwemo malipo ya ulinzi kwa Taasisi ya UMAWA, ununuzi wa mafuta pamoja na ununuzi wa vifaa vya kutendea kazi.

**Programu Kuu P00202: Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu**

**Matokeo ya Muda Mrefu:** Kukuza upatikanaji na Ufikiwaji wa Huduma kwa Watu wenye Ulemavu

51. **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ilipangiwa kiasi cha TZS. 1,563,990,000 ambapo hadi kufikia Machi, 2025 imepatiwa Ruzuku ya TZS. 761,939,243.5 ambapo (Mishahara 490,228,846.5 na Matumizi ya Kawaida 271,710397) sawa na asilimia 49.

52. **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa kipindi cha mwaka 2025/2026, imetekeleza yafuatayo:-

a) Afisi imewalipia ada ya masomo ya muda mrefu wafanyakazi wanne (4) na ada ya masomo ya muda mfupi mfanyakazi mmoja (1). Aidha, watumishi wawili wamepatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA). Afisi pia imeendelea kuwajengea uwezo waratibu wa mitandao ya Wilaya ya Watu wenye Ulemavu (CBID Network) unguja na Pemba ambapo jumla ya watu 1,343 wameungwa katika mitandao hiyo ili kutatua changamoto zinazowakabili Watu wenye Ulemavu.

b) Afisi kwa kushirikiana na Madrasa Early Childhood Progamme iliendesha mafunzo ya siku moja kwa wajumbe wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu yaliolenga kuwajengea uelewa juu ya dhana ya ujumuishwaji pamoja na kuutambulisha mradi wa CADiR unaotekelezwa kwa muda wa miaka mitano (2024-2028).

c) Afisi imeandaa maandiko manne ya miradi ikijumuisha mradi wa Kuanzisha Kituo cha Marekebisho ya Masuala ya Watu wenye Ulemavu, Uwezeshaji kiuchumi kwa Watu wenye Ulemavu, Afya ya Uzazi na Uzazi wa Mpango Kwa vijana wenye Ulemavu – Zanzibar na Ushiriki wa Watu wenye Ulemavu katika nafasi ya Uongozi kwa lengo la kutafuta fursa za kuwawezesha Watu wenye Ulemavu. Aidha, maandiko hayo tayari yamewasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na baadhi ya wadau wa maendeleo wa masuala ya watu wenye ulemavu kwaajili ya kutafutiwa fedha za utekelezaji.

d) Afisi imeandaa rasimu ya awali ya Muongozo wa Mfuko wa Maendeleo wa Watu wenye Ulemavu Zanzibar ambapo wadau mbali mbali wa taasisi na Serikali ikijumuisha, Jumuiya za Watu wenye Ulemavu na wataalamu kutoka Wizara ya Afya walitoa maoni yao. Aidha, katika lengo la kuimarisha Mfumo wa taasisi wa Baraza, jumla ya watu 88 (55 wanawake na 33 wanaume) walishiriki kuandaa Muundo wa Utumishi wa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu katika Afisi ya Kamisheni ya Utumishi wa Umma. Pia, Baraza kwa kushirikiana na Tume ya Mipango chini ya Ufadhili wa UNFPA limekusanya maoni ya wadau 232 kutoka katika taasisi za Serikali, Jumuiya za Watu wenye ulemavu, Asasi za kiraia na watu mashuhuri (Unguja 124 (wanawake 57

na wanaume 67) na Pemba watu 108 (wanawake 41 na wanaume 67) juu ya Mpango Mkakati wake wa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2026 hadi 2030 ambapo rasimu ya awali ya Mpango huo imetayarishwa.

e) Afisi imetoa elimu kwa umma juu ya haki za watu wenye ulemavu katika ushiriki na ushirikishwaji kuelekea uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025, ambapo jumla ya vipindi 13 vimerushwa hewani, kupitia redio, TV na Magazeti. Elimu juu ya masuala ya Watu wenye Ulemavu ikiwa ni pamoja na masuala ya Udhalilishaji, utumiaji wa Vifaa saidizi, Mfuko wa Maendeleo ya Watu wenye ulemavu, Uandikishaji wa watoto wenye ulemavu maskulini, uwepo wa Mabaraza ya Wilaya pamoja na fursa za mikopo kwa watu wenye ulemavu imetolewa kupitia Maonyesho ya Kilimo yaliyofanyika Dole Wilaya ya Magharibi A, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja ambapo jumla ya wananchi 449 (wanaume 256 na wanawake 192) ikiwemo wanafunzi wa shule za msingi na sekondari na Viongozi walitembelea banda la Afisi.

f) Afisi kwa kushirikiana na Taasisi ya ***Qatar Charity Organization, Emarate leasure,*** na ***All about albinisim,*** imetoa ruzuku kwa watu 17 kutoka Pemba (Wanaume 13 na Wanawake 4) pamoja na kugawa vyerehani 60 kwa vikundi vinne vya Watu wenye Ulemavu ili viweze kuwawezesha kiuchumi

katika harakati zao za Maisha ya kila siku. Aidha, Afisi imeratibu upatikanaji wa vifaa saidizi 773 (Motor Wheelchair 60, Sun screen 377, kofia 236 na miwani 100). Vilevile, Afisi imesimamia upatikanaji wa Vitambaa 350, Nyuzi 200, Mikasi 50, Zipu 1,250, Meza 50, Viti 50, Visanduku 50, viti vya watoto wenye ulemavu 50, magodoro 11, boksi za pempas 5 na vitanda vitano. Aidha, afisi imepokea na kuzigawa mashine 33 za kusagia nafaka. Thamani ya vifaa hivyo ni jumla ya shilingi 1,435,672,000. Vifaa hivyo vimekabidhiwa kwa wahusika ambapo jumla ya vikundi 5 walipatiwa vifaa hivyo. Aidha, kwa. Kiambatanisho nambari 4 kinafafanua.

g) Afisi imetoa elimu kwa umma juu ya haki za watu wenye ulemavu katika ushiriki na ushirikishwaji kuelekea maadhimisho ya siku ya Watu wenye ulemavu Duniani tarehe 3/12/2025, ambapo jumla ya vipindi 15 vimerushwa hewani, kupitia Radio, TV, na mitandao ya Kijamii.

h) Afisi imefanya ukaguzi wa miundombinu rafiki kwa watu wenye ulemavu kwa majengo 10 ya umma kupitia Wizara tano (5) za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa upande wa Pemba. Ukaguzi huo umeonesha kuwa kwa wastani wa majengo hayo yamezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu ingawa baadhi ya majengo hayo yanahitaji marekebisho madogo madogo ili kuzingatia Muongozo wa Kitaifa wa viwango vya

Miundombinu rafiki kwa Watu wenye Ulemavu. Aidha, Afisi imewasilisha changamoto hizo kwa taasisi husika kwa ajili ya marekebisho. ***Kiambatanisho nambari 5 Kinahusika.***

i) Huduma za utawala na uendeshaji wa Afisi zimetolewa zikiwemo malipo ya umeme, mafuta, ununuzi wa vifaa vya usafi, ukarabati wa vyoo pamoja na matengenezo ya gari. Vilevile, watumishi watano (5) wamepatiwa stahiki zao za likizo, ubani kwa watumishi wawili (2), malipo ya posho la kazi maalum kwa watumishi watano (5) pamoja na upimaji wa utekelezaji wa majukumu kwa watumishi 22 ambapo watumishi wawili wamepandishwa daraja na watumishi 20 wamepatiwa nyongeza za mwaka.

**Programu Ndogo S0020302: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

**53.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (S0020302) ya Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti ina lengo la Kusimamia utekelezaji wa Mipango, Miradi ya maendeleo na Bajeti. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu imetengewa kiasi cha **TZS. 281,335,713**. Hadi kufikia Machi, 2026 imepatiwa kiasi cha **TZS. 175,219,386** (**Mishahara TZS. 125,321,575** na Matumizi mengineyo **TZS. 49,897,81**1) sawa na asilimia 62.

**54.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

a) Afisi kwa kushirikia na Taasisi ya Uongozi pamoja na Asasi ya kiraia ya CAN Tanzania imeratibu uandaaji wa Sera ya mazingira, Mpango wa Utekelezaji na Mpango wa Ufuatiliaji na Tathmini wa sera hiyo ambayo tayari imewasilishwa kwa sekretarieti ya Makatibu wakuu.

b) Afisi kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imefanya ziara ya ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo kwa Unguja na Pemba katika maeneo ya Weni na Msingini Chakechake kwa kuangalia utekelezaji wa mpango wa kuirithisha Zanzibar ya Kijani, Tovuni Pemba, Mwanakombo, Matemwe pamoja na Bumbwini Mafufuni kwa ajili ya kuangalia hatua zilizofikiwa kiutekelezaji sambamba na kubaini changamoto zilizojitokeza.

c) Afisi imeandaa Mpango wa Utekelezaji wa miaka mitano kwa kuzingatia ahadi za Mheshimiwa Rais alizozitoa katika kipindi cha kampeni za uchaguzi 2025, maagizo ya Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi wa Baraza la 12 la Wawakilishi 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2025- 2030, Dira ya Maendeleo ya 2050 na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP).

d) Afisi imeandaa ripoti ya ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi kwa kipindi cha Julai 2025 – Machi 2026 na kuwasilishwa Tume ya Mipango, Ilani ya CCM kwa kipindi cha siku 100 za Uongozi wa Rais wa Zanzibar na Spika wa Baraza la Mapinduzi Mhe. Dkt Hussein Ali Mwinyi pamoja na ripoti za Kamati

ya Bajeti kwa kipindi cha nusu mwaka Julai hadi Disemba 2026, Kamati ya Kusimamia Viongozi wa Kitaifa kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2026 pamoja na ripoti yar obo ya tatu (Januari hadi Machi 2026) na kuziwasilishwa kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kama ilivyoelekezwa. Aidha, Afisi ilifanya ziara ya ufuatiliaji wa mradi wa kusafisha maji machafu uliopo msingini Chakechake Pemba kwa lengo la kukagua hatua za mwisho za kazi zilizopangwa kutekelezwa ambapo shughuli zote tayari zimeshatimia.

e) Afisi imeendelea kuwajengea uwezo watendaji wa Idara kwa kuwapatia vitendea kazi ikiwemo kompyuta tatu (3) na projekta moja (1) na wafanyakazi wawili wa Idara walipatiwa mafunzo ya siku tano kuhusiana na uandaaji na uandishi wa utafiti.

**Programu Ndogo S0020301: Utumishi na Uendeshaji**

**55.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (S0020301) ya Utumishi na Uendeshaji ina lengo la Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma za Afisi. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu ilipangiwa **TZS.1,127,864,473** ambapo **(TZS.594,322,945** kwa ajili mishahara na **TZS 533,541,528** kwa matumizi mengineyo).Hadi kufikia mwezi Machi, 2026 kiasi cha **TZS. 911,998,822** zimepatikana (Mishahara **TZS.655,430,792** na Matumizi mengineyo **TZS.256,568,030**) sawa na asilimia 81 ya utekelezaji wa programu.

**56. Mheshimiwa Spika,** Programu hii imetekeleza yafuatayo:-

a) Huduma mbalimbali za utawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo stahiki za malipo baada ya saa za kazi kwa watumishi 13, malipo ya posho la likizo la kawaida kwa watumishi 30 (W'me 12 na W'ke 18), ununuzi wa vitendea kazi, vifaa vya kuandikia, vifaa vya gari, vifaa vya usafi, malipo ya umeme na mafuta. Vilevile, Afisi imewafanyia upimaji wa utendaji kazi watumishi 27 ambapo watumishi 14 wamepandishwa daraja, na watumishi 13 wamepatiwa nyongeza za mwaka.

b) Afisi inaendelea kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi wanne ambapo wawili wanaendelea na masomo yao (mmoja katika fani ya Uchumi na Fedha na mwengine katika ya Rasilimali Watu) na kwa watumishi wawili wapya (mmoja katika fani ya teknolojia ya mawasiliano na mwengine katika fani ya Rasilimali watu). Aidha, Watumishi 11 wapya (wanaume 8 na wanawake 3) wamepatiwa mafunzo ya awali katika Chuo cha Utawala wa Umma (IPA). Vilevile, safari za viongozi na maafisa zilizowawezesha kushiriki mikutano mbalimbali ndani na nje ya Zanzibar ikijumuisha Pemba, Dar es salaam, Dodoma, Morogoro na Arusha zimegharamiwa. Aidha, ujenzi wa jengo la Afisi lenye vyumba vinne (4) na ununuzi wa samani umekamilika katika eneo la Afisi ya Makamu wa kwanza wa Rais Migombani

na kuanza kutumika na kutatua changamoto ya uhaba wa nafasi kwa watumishi.

c) Afisi imeratibu vikao sita (6) vya bodi ya zabuni na Tathmini ya zabuni za ununuzi, mkaguzi wa ndani wa hesabu, Kamati tendaji na Kamati ya Uongozi.

d) Afisi imeratibu na kufanikisha safari za watendaji na Viongozi Unguja na Pemba kwa ajili ya kushiriki utekelezaji wa majukumu ya Wizara na taasisi zake ikiwemo kazi za kamati na ufuatiliaji wa kazi za kawaida umefanyika ambapo jumla ya safari nne zimegharamiwa.

**Programu Ndogo S0020303: Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba**

**57.** **Mheshimiwa Spika,** Programu Ndogo (S0020303) ya Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba ina lengo la Kuimarisha mazingira ya kufanyia kazi na utoaji wa huduma kwa Afisi kuu - Pemba. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Programu imetengewa kiasi cha **TZS.820,227,088** hadi kufikia mwezi Machi, 2026 imepatiwa kiasi cha **TZS. 713,927,079** (**TZS.513,834,000** kwa ajili ya mishahara **TZS.200,093,079** kwa matumizi mengineyo) sawa na asilimia 87 ya utekelezaji wa programu.

**58.** **Mheshimiwa Spika,** Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 Programu imetekeleza yafuatayo: -

a) Afisi kwa kushirikiana na Tume ya Mipango imefanikisha ziara ya pamoja kutembelea miradi ya mazingira inayohusiana na mabadiliko ya tabianchi kwa lengo la kutathmini hatua za maendeleo ya miradi iliyotekelezwa na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Miradi iliyotembelewa ni mradi wa ujenzi wa tuta la kuzuia maji ya chumvi kuingia katika maeneo ya kilimo Tovuni, ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari Kisiwa Panza, Msuka na Kojani. Vilevile, Afisi imefanya ukaguzi wa maeneo yanayoathiriwa na mabadiliko ya tabianchi, maeneo yaliyokaguliwa ni Mtambwe Mkuu, Mtangani, Gando na Tibirinzi, lengo la ukaguzi ni kuyatambua na kuyaweka katika mpango wa kuyapatia ufumbuzi maeneo hayo.

b) Afisi imeratibu ziara za Mheshimiwa Kaimu Waziri wa Nchi Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ajili ya kujitambulisha na kufanya mazungumzo na watumishi Afisi Pemba na kutembelea Afisi ya Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Pujini. Katika ziara hiyo Mheshimiwa alitembela mradi wa kusafisha maji machafu Msingini.

c) Huduma za utawala na uendeshaji zimetolewa zikiwemo malipo ya posho la likizo kwa watumishi 7, nyongeza ya mshahara baada ya kupimwa utendaji kazi wao kwa watumishi 12 na fedha za ubani kwa watumishi wawili (2). Vilevile, watumishi 6 wamelipiwa ada za masomo ya muda mrefu

na watumishi 5 wamelipiwa ada za masomo ya muda mfupi. Afisi imegharamia malipo ya maji, umeme, mafuta, vifaa vya kuandikia pamoja na matengenezo ya gari.

**Programu Kuu: P00204 Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais**

**Matokeo ya muda mrefu:** Upatikanaji wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais

**59.** **Mheshimiwa Spika,** Programu hii Kuu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 ilipangiwa kiasi cha **TZS.931,377,131**. Hadi Machi, 2026 imepatiwa matumizi ya kiasi cha **TZS.580,206,503.5** (**TZS. 490,709,197.5** Mishahara na Matumizi ya Kawaida **TZS. 89,497,306)** sawa na asilimia 62 ya utekelezaji programu.

**60.** **Mheshimiwa Spika,** Programu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais imetekeleza yafuatayo:-

a) Afisi imefanikisha safari za Muheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais ndani na nje ya Zanzibar ambapo jumla ya safari 17 zimeratibiwa.

b) Afisi imesimamia upatikanaji wa huduma za ofisini na nyumbani kwa Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais kwa kuwapitia vitendea kazi, mafuta, vifaa vya kuandikia, stahiki za wafanyakazi, kufanya matengenezo madogo madogo ya vyombo vya moto, kulipa bima na leseni za barabarani na ununuzi wa vifaa vya magari.

## C. UTEKELEZAJI WA BAJETI ZA TAASISI ZINAZOSIMAMIWA NA WIZARA KWA JULAI, 2025 – MACHI,2026

**FUNGU B04 (USIMAMIZI WA MAZINGIRA)**

**PROGRAMU KUU P03401: Usimamizi wa Mazingira**

**Matokeo ya muda mrefu:** Kuimarisha usimamizi wa mazingira

**61. Mheshimiwa Spika,** fungu hili lina Progamu Kuu mbili na ndogo tatu (SB040101,SB040102 na SB040201)

**62. Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 Programu hii iliidhinishiwa **TZS. 3,085,100,000** katika utekelezaji wa majukumu yake. Kati ya fedha hizo **TZS.1,196,100,000** ni kwa ajili ya mshahara, na **TZS.736,900,000** kwa matumizi mengineyo na **TZS.1,152,100,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Hadi Machi, 2025, **TZS.2,429,676,000**zilipangwa kutumika ambapo jumla ya **TZS.1,236,520,808** zilipatikana (**TZS. 929,989,519.50** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 260,564,134** kwa matumizi mengineyo**)** zilipatikana sawa na asilimia 51 na **TZS.45,967,155** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. ***Kiambatanisho nambari 2 kinafafanua.***

a) Katika kupunguza athari za kimazingira na kiafya zinatokana na mifuko ya plastiki, operesheni 57 (28 Unguja, 29 Pemba) sawa na asilimia 42.2 ya operesheni 135 (81 Unguja na 54 Pemba)

zilizopangwa zimefanyika. Kupitia operesheni hizo jumla ya watu 68 (Unguja 47, Pemba 21) walikamatwa na kilogramu 2,265.75 (Unguja 1,734.25 Kg, Pemba 531.5 kg) za mifuko ya plastiki na kutozwa faini ya Shilingi 9,605,000 (Unguja 8,290,000 na Pemba 1,315,000) ambazo zilingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

b) Katika kupunguza uharibifu wa maliasili zisizorejesheka, Afisi imefanya operesheni 44 (Unguja 26 na Pemba 18) ambayo ni sawa na asilimia 33.3 ya operation 135 zilizopangwa. Kupitia operesheni hizo watu watatu (3) wakiwa na gari za ng'ombe zilizobeba mchanga kinyume na taratibu na watu wawili wenye gari moja kwa upande wa Unguja walikamatwa na kufikishwa katika Mahakama ya Mwanzo, Manispaa ya Mjini na kutozwa faini ya Shilingi 1,000,000 ambazo zimeingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali. Kwa upande wa Pemba mtu mmoja (1) alikamatwa katika Shehia ya Ole, Wilaya ya Chake Chake kwa kosa la kukata mti wa muembe bila kufuata taratibu na kutozwa faini ya Shilingi 300,000.

c) Katika jitihada za kupunguza uharibifu na uchafuzi wa mazingira kwa jamii, Afisi imefanya ufuatiliaji wa maeneo 202 (Unguja 151 na Pemba 51) sawa na asilimia 112.2 ya maeneo 180 (Unguja 108, Pemba 72) yaliyopangwa. Kupitia ufuatiliaji huo, miongozo ya kimazingira ilitolewa

kwa maeneo husika ili kusaidia kupunguza kero, uchafuzi na uharibifu wa mazingira uliobainika. ***Kiambatanisho nambari 6 kinafafanua***.

d) Katika kuhakikisha kuwa miradi ya kiuchumi na kimaendeleo inatekelezwa kwa kuzingatia kanuni, masharti na miongozo ya kimazingira, Afisi ilifanya ufatiliaji wa miradi 103 (Unguja 47, Pemba 56) sawa na asilimia 57 ya miradi 180 (Unguja 108, Pemba 72) iliyopangwa. Ufuatiliaji huo ulionesha kuwa asilimia 85 ya miradi imezingatia masharti na miongozo ya kimazingira iliyotolewa na asilimia 15 ya miradi ilibainika kutokutimiza masharti ya kimazingira na hivyo kutakiwa kutimiza masharti husika kwanza kabla ya kuendelea na shughuli zake. Kiambatanisho nambari 7 kinafafanua.

e) Afisi katika kuhakikisha kuwa miradi ya uwekezaji na maendeleo inazingatia masuala ya mazingira kabla ya kuanza utekelezaji wake ilipanga kufanya tathmini 131 za kimazingira (Unguja 83, Pemba 48) ambapo tathmini 123(100 Unguja na 23 Pemba) zilifanyika sawa na asilimia 94 ya malengo yaliyopangwa. Vyeti vya Tathmini za Kimazingira vilitolewa kwa miradi husika. ***Kiambatanisho nambari 8*** kinafafanua kinaonesha mchanganuo wa aina za Tathmini za Kimazingira zilizotekelezwa.

f) Katika jitihada za kukuza uelewa na ushiriki wa jamii kuhusu masuala ya uhifadhi wa mazingira, Afisi imerusha hewani vipindi 10 vya TV na

vipindi vya redio vinavyohusiana na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira, mvua za vuli na mazingira, maendeleo ya Serikali ya awamu ya Nane kupitia shughuli za uhifadhi na usimamizi wa mazingira Zanzibar, muongozo wa uanzishaji na uendeshaji wa viwanda vya matofali na umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na upandaji wa miti, Maendeleo na mazingira, Nishati safi na mazingira, udhibiti na uharibifu wa mazingira, na Utekaleaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM wa 2025-2030 katika sekta ya mazingira. Vilevile, Afisi imeandaa na kusambaza ujumbe wa kimazingira kupitia mitandao ya kijamii kwa lengo la kuongeza uelewa na kuhamasisha jamii kushiriki katika kulinda mazingira, kukuza mwamko kwa jamii katika kuchukua hatua za uhifadhi wa mazingira na kuendeleza kampeni ya kujenga Zanzibar ya kijani.

g) Afisi imeendelea kutoa huduma za utawala na uendeshaji kwa kuwapatia watumishi 17 posho la likizo la kawaida, watumishi 19 walipata nyongeza ya mshahara ya mwaka baada ya kufanyiwa upimaji, watumishi 8 waliolipiwa ada ya mafunzo ya muda mfupi na watumishi 10 wanaendelea kulipiwa masomo ya muda mrefu katika vyuo mbalimbali. Afisi pia imefanya malipo ya umeme, ununuzi wa mafuta, vifaa vya matengenezo madogo ya gari, vifaa vya kuandikia, kompyuta na vifaa vya usafi. Aidha, tovuti ya afisi imeimarishwa kwa kuwekwa

mfumo mpya wa kisasa ulioandaliwa na e-GAZ ili kuongeza urahisi wa upatikanaji wa taarifa, muonekano wa kitaalamu pamoja na usalama wa taarifa zinazochapishwa mtandaoni.

h) Afisi ilifanya kikao kimoja cha dharura cha Bodi ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa ajili ya kujadili, kutoa maoni na kupitisha ripoti ya kufunga hesabu za mwaka wa fedha 2024/2025 ambayo iliwasilishwa Afisi ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama taratibu na miongozo ya Serikali inavyoelekeza.

i) Afisi imesimamia uteketezaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo tani 30 za nyaraka kutoka taasisi mbalimbali katika maeneo ya Muungoni na Kibele, tani 3 za maziwa kutoka Kampuni ya Lusa Trade, Lita15,840.0 za Bia ambazo zinamilikiwa na kampuni ya ZMMI, Chipsi za mbatata tani 24.36, maziwa tani 1.6 za Kampuni ya Majani Traders pamoja na Tani 202.8 za sukari ya BRAZILIAN BROWN SUGAR ya Kampuni ya H and Y Enterprises (TZ) Ltd baada ya kuthibitika kuwa bidhaa hizo hazifai kwa matumizi ya binadamu. Lengo la uteketezaji huu ni kulinda afya ya jamii kutokana na matumizi ya bidhaa zisizofaa na kupunguza athari za mazingira zinazoweza kutokea kutokana na matumizi ya bidhaa zilizoharibika.

j) Afisi kwa kushirikiana na Shirika la Kimataifa la Uhifadhi wa Mazingira (IUCN) na wadau wengine iliadhimisha siku ya Usafi Duniani tarehe 20 Septemba 2025, ambapo kupitia maadhimisho hayo ilihamasisha jamii na kufanya usafi katika eneo la Kwarara, Wilaya ya Magharibi B, Mkoa wa Mjini Magharibi pamoja na kutoa elimu ya kutenganisha taka zinazooza na zisizooza ambapo jumla ya tani 10 za taka zilikusanywa ikijumuisha tani 1 ya taka za plastiki.

k) Afisi ilifanya ziara ya kimasomo katika Baraza la Taifa la Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira Dar es Salaam (NEMC) iliyolenga kuimarisha mashirikiano na kujifunza masuala ya kimazingira yanayosimamiwa na baraza hilo pamoja na kuandaa Rasimu ya Hati ya Makubaliano (MoU) baina ya ZEMA na NEMC na Bodi 'Chater' ya ZEMA. Aidha, Afisi ilifanya kikao cha mashirikiano kilichofanyika Zanzibar baina ya ZEMA na NEMC chenye lengo la kubalidishana uzoefu juu ya tathmini za kimazingira.

**l) FUNGU C04: MAMLAKA YA UDHIBITI NA KUPAMBANA NA DAWA ZA KULEVYA**

**PROGRAMU KUU P03201: Udhibiti wa dawa za kulevya**

**Matokeo ya muda mrefu:** Jamii kuepukana na matumizi ya dawa za kulevya

**63.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 Programu hii iliidhinishiwa **TZS. 8,740,600,000.** Kati ya fedha hizo **TZS. 2,133,800,000** kwa ajili ya mishahara, shilingi 2,106,800,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 4,500,000,000** ni kwa ajili ya kazi za maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya **TZS. 7,744,469,000** zilipangwa kutumika ambapo jumla ya **TZS. 2,433,968,155** zilipatikana sawa na asilimia 31 (**TZS. 1,553,631,155** sawa na asilimia 97 ni kwa ajili ya mishahara na **TZS. 880,337,000** sawa na asilimia 54 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Kiambatanisho nambari 2 kinafafanua.

**64.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii imetekeleza mambo yafuatayo: -

a) Afisi imefanya operesheni 224 (Unguja 164, Pemba 80) za kiintelijensia kati ya 200 zilizopangwa ambazo ni sawa na asilimia 112 na kufanikiwa kufungua kesi 164 (Unguja 136, Pemba 28) ambapo watuhumiwa 199 (wanaume 177, wanawake 23) waliohusishwa na makosa ya usambazaji na usafirishaji wa dawa za kulevya walikamatwa.

b) Afisi imezishughulikia kesi 44 (Unguja 29, Pemba 15) ambapo kesi 20 zimepata hatia na kesi 24 zimeachiliwa huru kwa sababu mbali mbali zikiwemo kutokuunganika mnyororo wa ushahidi

(chain of custody) na kesi 201 (Unguja 197, Pemba 4) zinaendelea Mahakamani.

c) Katika kuendeleza jitihada za kuzuia na kudhibiti matumizi na usafirishaji wa dawa za kulevya, Afisi imeendelea kutoa elimu kwa jamii kupitia njia mbalimbali ambapo jumla ya vipindi 12 vya redio na televisheni vilirekodiwa na kurushwa hewani kupitia vituo vya Coconut FM, Mjini FM, ZBC Redio na ZBC Televisheni pamoja na kufanyika kwa mikutano miwili ya Waandishi wa habari (Press confress) kuhusiana na tamko la utaifishaji wa mali za mtuhumiwa wa uhalifu wa dawa za kulevya. Vilevile, elimu ilitolewa katika taasisi za elimu kwa kuwafikia wanafunzi na walimu 8,225 (wanaume 3851 na wanawake 4374), katika maeneo ya kazi kwa kuwafikia vijana 872 (wanaume 492 na wanawake 380), kuwafikia askari wanafunzi 1,332 (wanaume 942 na wanawake 390). Wanajamii ,1699 katika shehia 8 za Unguja na Pemba (Welezo,Magirisi, Mjimbini, Mtoni kidato, Jang'ombe, Tibirinzi na Pujini) Elimu hii imelenga kuwawezesha wananchi, hususan wanafunzi na wafanyakazi, kuelewa kwa kina kuhusu aina za dawa za kulevya, madhara yake kiafya, kijamii na kisheria.

d) Waraibu 39 wanaendelea kupatiwa huduma za tiba na marekebisho ya tabia katika Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia Kidimni na familia 170 za vijana wanaopata huduma

katika kituo hicho walipatiwa huduma ya tiba ya kifamilia (family therapy). Vilevile, waraibu 68 wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali ikijumuisha ufugaji ng'ombe, kilimo cha vitalu nyumba (green house), ufundi charahani na gereji ili kuwawezesha kujitegemea kiuchumi na kuepuka kurudia katika matumizi ya dawa za kulevya na waraibu wapya 143 walipokelewa kituoni hapo.

e) Afisi ilifanya Ziara ya ushirikiano na Afisi ya TAKUKURU– Dodoma kwa lengo la kubadilishana uzoefu, kuimarisha ushirikiano wa kikazi na kujenga uwezo wa watendaji, watumishi 6 walishiriki na kujifunza kuhusu mifumo bora ya uendeshaji wa Kituo cha Mawasiliano (Call Centre) na matumizi ya teknolojia katika kupokea na kushughulikia taarifa za uhalifu kutoka kwa jamii.

f) Afisi iliratibu na kushiriki katika vikao kazi mbalimbali vilivyohusisha Masheha wa Wilaya ya Wete, Mjini, na Magharibi B, DPP na Mahakama, Kamati ya Ulinzi na Usalama Wilaya ya Mjini na Jumuiya ya Maimamu, Polisi Jamii – Wilaya ya Magharibi A, Wizara ya Afya, Walimu na wazazi wa Skuli ya Mwanakwerekwe A, vyenye lengo la kuimarisha mashirikiano katika mapambano na udhibiti wa dawa za Kulevya. Aidha, Watumishi wawili walishiriki mikutano ya kimataifa yenye lengo la kupanga mikakati na kushirikiana katika kupambana na uhalifu wa kupangwa na mtumishi

mmoja kushiriki kikao cha 51 cha Kikosi Kazi cha Maafisa Wakuu na kikao cha 25 cha Baraza la Mawaziri wa Jumuiya ya ESSAAMLG kilicholenga kujadili mbinu za pamoja katika kudhibiti utakatishaji wa fedha haramu katika ukanda wa Kusini na Mashariki mwa Afrika.

g) Afisi imeanzisha Kituo cha mawasiliano ya dharura kwa kurahisisha utoaji wa taarifa kutoka kwa wananchi kuhusu uhalifu wa dawa za kulevya. Lengo ni kuiwezesha jamii kuripoti matukio au viashiria vya uhalifu wa dawa za kulevya wakati wowote kwa haraka na usiri kwa kutumia namba ya bure 119. Hadi sasa jumla ya simu 295 zimepokelewa kuripoti taarifa mbalimbali za uhalifu wa dawa za kulevya ambapo taarifa 167 sawa na asilimia 57 zimefanyiwa kazi na kufanikisha kuwakamata wahalifu na taarifa 128 zinaendelea na uchunguzi.

h) Afisi imefanya mafunzo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Afisi za Viongozi wakuu wa Kitaifa kwa kutoa uelewa zaidi juu ya majukumu, mafanikio na changamoto zinazoikabili Mamlaka na kuchukua ahadi ya kuisaidia Mamlaka ili iimarishe utekelezaji wa majukumu yake na kuleta ufanisi zaidi katika mapambano dhidi ya dawa za kulevya na kuhakikisha Zanzibar inakuwa salama.

**Programu Kuu P03202** : Utawala na Rasilimali Watu wa Mamlaka ya Dawa za Kulevya

**Matokeo ya muda mrefu :** Kuweka mazingira bora ya kazi ili kuongeza ufanisi katika utendaji kazi

Programu hii Kuu ina lengo la kuweka mazingira mazuri ya kazi na kuendesha shughuli za Mamlaka.

**65.** **Mheshimiwa Spika,** kwa kipindi cha mwaka 2025/2026 Programu hii iliidhinishiwa **TZS.2,379,172,000** katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo **TZS.722,004,284** kwa ajili ya mishahara na **TZS 537,641,250** kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS,568,075,250** kwa ajili ya kazi za maendeleo. kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026 jumla ya **TZS.1,827,727,784** zilipangwa kutumika na **TZS.1,239,065,029** zimepatikana ambapo **(TZS.603,144,662** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS.244,695,407** matumizi mengineyo na kazi za maendeleo imepata **TZS.391,224,960)** sawa na asilimia 68. ***Kiambatanisho nambari 2 kinafafanua.***

**Programu hii imetekeleza yafuatayo: -**

a) Afisi imelipa stahiki za wafanyakazi ikiwemo mishahara, malipo ya likizo kwa watumishi 8, pamoja na kugharamia huduma za usafiri. Aidha, malipo ya umeme, magazeti ya Serikali, safari za kikazi zimelipiwa ndani na nje kwa ajili ya kuweka mazingira bora ya kazi yenye kuleta ufanisi.

b) Afisi katika kuimarisha utendaji kazi imewapatia mafunzo ya muda mfupi watumishi 122 katika fani mbali mbali yanayohusu miongozo ya ukamataji, uchunguzi wa kisayansi (forensic science), utunzaji wa vielelezo, ukusanyaji wa ushahidi wa kielektroniki, ukaguzi wa makontena, na kusimamia mashahidi Mahkamani. Aidha, Watumishi 15 walipatiwa mafunzo ya awali kwa waajiriwa wapya na watumishi 47 wamepatiwa mafunzo ya afya na usalama kazini, utunzaji wa kumbukumbu na Nyaraka.

**FUNGU C05:TUME YA UKIMWI**

**66.** **Mheshimiwa Spika,** fungu hili lina programu kuu mbili kama ifuatavyo

**Programu Kuu C0501: Programu Kuu ya Kuratibu Mwitiko wa Taifa Wa UKUMWI**

**Matokeo ya muda mrefu:** Kiwango cha maambukizo ya VVU kupungua kutoka 0.4% hadi 0.2% ifikapo 2030 nchini.

**67.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2025/2026 Programu hii kuu iliidhinishiwa **shilingi 2,379,172,000** katika utekelezaji wa majukumu yake ambapo **shilingi 783,200,000** kwa ajili ya mishahara na 748,200,000 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya **shilingi 1,239,065,026** ambapo (Mishahara ni **shilingi 603,144,662** na Matumizi ya Kawaida ni **shilingi 244,695,504**) zilipatikana sawa na asilimia 68 kwa ajili ya utekelezaji wa programu zake ndogo.

***Kiambatanisho namba 2 kinafafanua***.

68. **Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo (SC050101 na S0330102) ambazo ni Uratibu,Ufuatiliaji na Tathmini ya muitiko wa Taifa wa UKIMWI na mawasiliano na utetezi wa masuala ya UKIMWI

69. **Mheshimiwa Spika,** programu hii imetekeleza yafuatayo:-

70. **Mheshimiwa Spika,** Kupitia Programu hii, Afisi imefanya maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani tarehe 1 Disemba, kwa lengo la kuwaunga mkono wote wanaoishi na maambukizo ya Virusi vya UKIMWI na kutathmini jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na nchi yetu katika kukabiliana na janga la UKIMWI ambapo kauli mbiu kwa mwaka 2025 ilikuwa ***"TUVISHINDE VIKWAZO VYA KIFEDHA TUIMARISHE MAPAMBANO*** YA UKIMWI"

71. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imetoa elimu kwa makundi mbalimbali ya vijana kupitia mikutano ya wanafunzi wa vyuo vikuu, mitandao ya kijamii (Instagram, Facebook na TikTok) pamoja na redio na televisheni kwa lengo la kuongeza uelewa juu ya masuala ya UKIMWI, afya ya uzazi na stadi za maisha na kuepuka tabia hatarishi zinazoweza kuwaweka katika hatari ya kupata maambukizo ya VVU na maradhi ya kujamiiana. Pia, ililenga kuimarisha afya ya uzazi na kushajiisha matumizi ya huduma katika vituo vya huduma rafiki kwa vijana. Katika shughuli hizo jumla ya watu 94,727 wamefikiwa. ***Kiambatanisho nambari 9***

***kinafafanua***. Vilevile, Afisi imetengeneza mtandao wa kujifunza (e-learning) ambao utawasaidia vijana kupata taarifa mbalimbali juu ya UKIMWI, afya ya uzazi na stadi za maisha unaojulikana kwa jina la FUNGUKA.

**72.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanya mikutano 7 ya uratibu ambayo ni, Kamati ya Kitaifa ya Kondomu, mkutano wa wadau wanaofanyakazi na makundi maalum, mkutano wa wadau wa programu za vijana (vituo vya tiba, vituo Rafiki kwa vijana na Asasi za kiraia) na mkutano wa elimishaji rika wa vijana. Aidha, ziara mbili (2) zilizolenga kufuatilia utekelezaji wa masuala ya UKIMWI zilifanyika kupitia Taasisi zilizoratibiwa jumla ya watu 211,359 wamefikiwa. ***Kiambatanisho nambari 10A na B kinafafanua***.

**Programu Kuu 03302:** Programu Kuu ya Uratibu na Uendeshaji wa Tume ya UKIMWI
**Matokeo ya muda mrefu:** Kuimarika utendaji kazi ifikapo 2027

**73.** **Mheshimiwa Spika,** programu hii kuu kwa kipindi cha Julai 2025 hadi March 2026 ilidhiinishiwa jumla ya **shilingi 1,529,980,000** katika utekelezaji wa majukumu yake. Katika fedha hizo shilingi 596,933,570 ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 413,088,162** ni kwa matumizi mengineyo hadi Machi 2026 shilingi 780,389,991 zilipatikana ambapo shilingi 783,200,000 kwa ajili ya mishahara na shilingi 746,780,000 kwa matumizi mengineyo sawa na asilimia 51.

**74. Mheshimiwa Spika,** Programu ndogo (SC050201, SC050202 na SC050203) ambazo ni Uratibu na uendeshaji Pemba, Utawala na uendeshaji Unguja na Uratibu wa mipango, sera na utafiti.

**75. Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanya vikao 4 (Bodi ya Makamishna - 1, Bodi ya Manunuzi - 1 na Kamati ya Ukaguzi - 2) ili kusimamia uwajibikaji katika utendaji kazi na matumizi ya fedha za Serikali. Pia, Kitengo cha TEHAMA kimeendelea kufanya ukaguzi wa mfumo wa Afisi mtandao ili kuhakikisha wafanyakazi wanatumia mfumo huo wa Afisi Mtandao (e-Office) kwa ufanisi. Afisi imelipa stahiki za likizo kwa wafanyakazi 5 na kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa wafanyakazi 3. Afisi pia imelipia huduma za umeme, mtandao, ulinzi, usafiri, vifaa vya kiAfisi na matengenezo ya magari.

**76. Mheshimiwa Spika,** Afisi imeendelea kuratibu utekelezaji wa maazimio ya ya ESA (East and Southern African Commitment) yaliyoridhiwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambayo yanalenga kushughulikia changamoto zinazowakabili vijana wenye umri miaka 15- 24 katika masuala ya afya, jinsia na elimu, kuzuia na kupunguza mimba za mapema na zisizotarajiwa, udhalilishaji wa kijinsia, ndoa za mapema na maambukizo ya VVU. Watekelezaji wa Maazimio hayo ni sekta za serikali na Asasi za kiraia. Kwa kipindi cha Julai hadi Disemba 2025 jumla ya vijana 832,886 (Wanawake 423,511 na Wanaume

409,375) wamefikiwa kupitia taasisi mbalimbali kwa maeneo ambayo ESA inaelekeza.

77. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imeifanyia mapitio Sera ya Taifa ya UKIMWI ya mwaka 2012 ili ikidhi hali ya mabadiliko ya mwenendo wa maradhi, mabadiliko ya Kiuchumi na Kijamii nchini, maendeleo ya kisayansi na usimamizi na ushughulikiaji wa masuala ya UKIMWI ulimwenguni. Mchakato wa maandalizi wa sera hiyo uliwashirikisha wadau kutoka katika taasisi za serikali, binafsi, Asasi za kiraia na Washirika wa maendeleo. Rasimu hiyo imewasilishwa na kujadiliwa katika kikao cha kamati Tendaji ya Afisi ya Makamu wa Kwanza ya Rais.

78. **Mheshimiwa Spika,** Afisi imefanya mkutano ya kuhamasisha Sekta ya Utalii katika masuala ya UKIMWI kutokana na kuwepo uhusianao kati ya maambukizi ya VVU na ongezeko la vihatarishi vinavyoweza kupelekea kuongezeka kwa maambukizo nchini. Lengo la kuhamasihsa sekta hiyo ni kushiriki kikamilifu katika mwitikio wa taifa wa kupambana na VVU na UKIMWI na upatikanaji wa rasilimali kutoka sekta binafsi.

## D. MWELEKEO WA VIPAUMBELE VYA MATUMIZI YA WIZARA NA TAASISI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**79. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kusimamia masuala mtambuka yakiwemo usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya tabianchi, kusimamia upatikanaji wa haki na fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu, mapambano dhidi ya uingizaji, usafirishaji na utumiaji wa dawa za kulevya, kuimarisha upatikanaji wa kinga na tiba ili kumaliza maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI ifikapo 2030. Aidha, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ina dhamira ya kuimarisha utoaji wa huduma kwa kuzingatia Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya mwaka 2050, Mpango Mkuu wa maendeleo wa Taifa (ZADEP 2021/2026), Ilani ya Chama cha Mapinduzi 2025/2030, Malengo ya Maendeleo Endelevu ya Kitaifa (SDGs), Mikataba ya kimataifa, Sera, Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo na ahadi za viongozi wakuu wa Kitaifa.

## VIPAUMBELE VYA WIZARA NA TAASISI ZILIZO CHINI YA OMKR KWA MWAKA WA FEDHA WA 2026/2027.

**80. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha 2026/2027, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais imejipangia vipaumbele vifuatavyo: -

i. Kuendelea na juhudi za uhifadhi wa mazingira nchini kote kwa upandaji wa miti, matumizi ya

nishati salama, elimu ya mazingira, doria na kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kunusuru maeneo yanayongia maji ya Bahari (Ujenzi wa miundombinu himilivu kwa mabadiliko ya tabianchi) na kuimarisha harakati za kijamii na kiuchumi katika baadhi ya maeneo yaliyoathirika;

ii. Kujenga uelewa kwa jamii na wataalamu juu ya masuala ya biashara ya kaboni na kukaribisha uwekezaji;

iii. Kuimarisha mapambano dhidi ya dawa za kulevya kwa kuimarisha ukaguzi, uchunguzi pamoja na utoaji wa huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia kwa waathirika wa dawa za kulevya;

iv. Kuendelea kutoa haki na fursa sawa kwa maendeleo jumuishi ya watu wenye ulemavu nchini kwa kuimarisha Huduma za tiba, elimu na makaazi; na

v. Kuendeleza mapambano dhidi ya VVU na UKIMWI kwa lengo la kufikia azimio la kumaliza UKIMWI ifikapo 2030.

## MALENGO YA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**81.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imejipanga kutekeleza malengo yafuatayo:-

1. Kuratibu na kutekeleza shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais pamoja na kuimarisha

mashirikiano ya Kimataifa, Kikanda na kisekta baina ya SMZ, SMT na wadau wa maendeleo;

2. Kuwa na tafiti zitakazosaidia katika uandaaji wa mipango ya maendeleo ya muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu kwenye masuala yanayosimamiwa na Afisi;
3. Kuwa na watumishi wenye uwezo na watakaotekeleza majukumu yao kwa weledi na ufanisi;
4. Kuimarisha usimamizi na uhifadhi wa mazingira pamoja jitihada za kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa maendeleo endelevu Zanzibar;
5. Kuimarisha usimamizi na upatikanaji wa Haki na Fursa sawa kwa Watu wenye Ulemavu katika nyanja zote za Kijamii, Kisiasa na Kiuchumi;
6. Kuimarisha Udhibiti na Mapambano dhidi ya Uingizaji, Usafirishaji na Utumiaji wa Dawa za Kulevya ambao utaambatana na Mikakati madhubuti ya masuala ya Tiba na Marekebisho ya Tabia; na
7. Kuratibu muitiko wa Taifa wa UKIMWI nchini kwa kuongeza nguvu katika utoaji wa elimu masafa kwa makundi maalumu, vifaa tiba na dawa za kufubaza VVU.

**82.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais itaendelea kusimamia utekelezaji wa miradi nane (8) ya maendeleo kama ifuatavyo:-

i. Mradi wa kuirithisha Zanzibar ya kijani unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;

ii. Mradi wa kuibadilisha ZEMA kidigital (ZEMA digital transformation);
iii. Mradi wa (SCALE) wa Kuimarisha mifumo ya Kitaifa na kuziwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na athari za mabadiliko ya Tabianchi (WB);
iv. Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mbadiliko ya Tabianchi kwa jamii ya Pwani ya Zanzibar (Adaptation Fund);
v. Mradi wa kuimarisha jamii na mfumo wa Ikolojia katika kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika misitu ya miombo Tanzania Bara na Maeneo Kame ya Zanzibar (GEF/FAO);
vi. Mradi Shirikishi wa Kuhimili Mifumo ya Ikolojia ya Bahari na Ukanda wa Pwani na shughuli za kujipatia Kipato katika eneo la Kusini Mashariki Pemba (UNEP);
vii. Mradi wa ujenzi wa kituo cha tiba na marekebisho ya tabia Kangagani Pemba unaofadhiliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar;
viii. Programu jumuishi ya mabadiliko ya tabianchi na mazingira Zanzibar (ZJP) chini ya uhifadhi wa UNEP.

**83. Mheshimiwa Spika,** inasimamia mafungu makuu ya kibajeti manne (4) ambayo ni; 002 – Fungu la Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais (Afisi kuu), 034 – Fungu la Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira, 032 – Fungu la Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya na 033 – Fungu la Tume ya UKIMWI.

**84. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu saba (7) ambazo ni:-

I. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi;
II. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu;
III. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
IV. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais;
V. Programu ya Usimamizi wa Mazingira.
VI. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya;
VII. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI;

## MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

## MAKADIRIO YA MAPATO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**85. Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 imekadiriwa kukusanya jumla ya mapato ya jumla ya **TZS 854,019,000** kupitia vyanzo vyake viwili, ada ya uhifadhi wa mazingira na ada ya ukaguzi wa mazingira Unguja na Pemba chini ya usimamizi wa Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA). (Kiambatanisho nambari 12 kinahusika).

## MAKADIRIO YA MATUMIZI KWA PROGRAMU ZA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**86**. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais ili iweze kutekeleza programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 naiomba kamati yako iidhinishe jumla ya **TZS 35,558,539,602**. Kati ya fedha hizo **TZS. 17,529,000,000** kwa matumizi ya kawaida ambapo **TZS 7,453,567,000** kwa ajili ya Mishahara, **TZS 8,223,550,602** kwa matumizi mengineyo, na Ruzuku **TZS.1,906,039,000** kwa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu (**TZS. 788,539,000** kwa ajili ya mshahara na **TZS. 1,117,501,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo). Aidha, Afisi inaomba iidhinishiwe jumla ya **TZS .17,975,382,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **TZS. 15,750,000,000** kutoka SMZ na **TZS. 2,225,382,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo. ***(Kiambatanisho nambari 13 kinahusika)***

**87.** **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 itatekeleza malengo yake kupitia programu zake kuu saba (7) pamoja na makisio ya fedha kama ifuatavyo:-

i. Programu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 7,909,527,000**;

ii. Programu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 1,906,039,000**;

iii. Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 3,401,677,000**;

iv. Programu ya Uratibu wa Shughuli za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 1,622,009,000**; na

v. Programu ya Usimamizi wa Mazingira kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS. 4,931,467,000**

vi. Programu ya Udhibiti wa Dawa za Kulevya kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 13,274,460,000;**

vii. Programu ya Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa **TZS 2,682,479,602;**

**PROGRAMU KUU P01: URATIBU WA MABADILIKO YA TABIANCHI.**

**88.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu Kuu ya Uratibu wa Mabadiliko ya Tabianchi inaombewa jumla ya **TZS. 7,909,527,000**. Kati ya fedha hizo, **TZS. 432,286,000** ni kwa ajili ya mishahara**, TZS. 363,838,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na **TZS. 7,113,403,000** kwa ajili ya miradi ya maendeleo ambapo **TZS. 5,000,000,000**

kutoka kwa SMZ na **TZS 2,113,403,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**89. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kutayarisha Kanuni na Miongozo ya Kimazingira,
ii. Kufanya tathmini ya hali halisi ya mmong'onyoko wa fukwe kwa Unguja
iii. Kufanya vikao vya kamati ya ushauri vya Mazingira, pamoja na vikao vya kamati ya kitaalamu na kamati ya uongozi ya mabadiliko ya tabianchi,
iv. Kuandaa mandiko ya miradi ya kimazingira na mabadiliko ya tabiachi ,
v. Kukuza uelewa kwa jamii juu ya maswala ya mazingira na Mabadiliko Tabianchi kupitia Mikutano pamoja na vyombo vya habari
vi. Kufanya mkutano wa mashirikiano baina ya Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na Afisi ya Makamu wa Rais Muungano;
vii. Ujenzi wa miundombinu himilivu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi katika maeneo ya fukwe ili kuzuia maji ya bahari kuingia katika maeneo mbalimbali ya kilimo na makaazi kutokana na athari za Mabadiliko ya Tabianchi;
viii. Kuziwezesha halmashauri/Serikali za Mitaa 11 kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi;

ix. Kuratibu mikutano ya kamati za thathmini za maandiko ya miradi ya biashara ya kaboni na technolojia ya kisasa.
x. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji za kiafisi; na
xi. Kuandaa na kushiriki matukio ya kitaifa.

**PROGRAMU KUU P02: USIMAMIZI WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU.**

**90.** **Mheshimiwa Spika**, Programu Kuu ya Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu kwa mwaka wa fedha 2026/2027 inaombewa Ruzuku ya **TZS. 1,906,039,000**. Kati ya fedha hizo, **TZS.788,500,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS.1,117,539,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**91.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii, Afisi imepanga shabaha zifuatazo: -

i. Utawala na Uendeshaji wa Ofisi ya Baraza.
ii. Kufanya vikao vya Baraza la Taifa, Mabaraza ya Wilaya na Maafisa Waratibu wa Masuala ya Ulemavu.
iii. Kuandaa Maandiko ya Miradi, Mpango Mkakati na Muongozo wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu.
iv. Kufanya Ukaguzi wa Majengo na Mafunzo kwa (Wasafu, Wahandisi na Wakandarasi) wa Ujenzi katika Ufikiaji na Uzingatiaji wa Miundombinu rafiki kwa Watu Wenye Ulemavu.

v. Kufanya uhamasishaji na elimu kwa umma juu ya upatikanaji wa Haki na fursa kwa Watu Wenye Ulemavu kupitia Maadhimisho, Vipindi vya Redio na TV, Mitandao ya Kijamii, Machapisho, Mikutano ya Jamii na Mafunzo ya Ukalimani wa lugha ya Alama.

vi. Kufanya usajili na Kuwawezesha Watu Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Watu Wenye Ulemavu Zanzibar.

## PROGRAMU KUU P04: UENDESHAJI NA URATIBU WA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS.

**92.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu Kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais inaombewa jumla ya **TZS. 3,401,677,000** kati ya fedha hizo, **TZS. 1,885,875,000** ni kwa ajili ya mishahara na **TZS. 1,346,682,000** kwa ajili ya matumizi mengineyo na Ruzuku ya **TZS.169,120,000** kwa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu Pemba.

### Programu ndogo S0401: Utawala na uendeshaji

**93.** **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo ya Utawala na uendeshaji inaombewa jumla ya **TZS. 1,594,227,000** kati ya fedha hizo, **TZS. 920,905,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS.673,322,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**94. Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuratibu mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 20 na kuendelea kugharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 4;
ii. Kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo la Afisi;
iii. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa Afisi;
iv. Kufanya mapitio ya mkataba wa utoaji wa huduma kwa mtaka huduma;
v. Kuratibu vikao vya Afisi;
vi. Kuratibu safari za kikazi za ndani na nje ya nchi;
vii. Kusimamia na kuimarisha shughuli za habari na tehama, manunuzi, sheria, ukaguzi wa ndani na usimamizi wa fedha za umma kupitia mifumo ya kielektroniki; na
viii. Kulipa stahiki za wafanyakazi za Afisi.

**Programu ndogo S0402: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti**

**95. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo ya Uratibu wa Mipango, sera na utafiti inaombewa jumla ya **TZS. 373,345,000** kati ya fedha hizo, **TZS. 200,000,000** kwa ajili ya mishahara na **TZS. 173,345,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo

96. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

vii. Kuratibu maandalizi ya mipango na usimamizi wa utekelezaji wa shughuli za Afisi;

viii. Kuratibu tafiti za Afisi katika eneo la mazingira na mabadiliko ya tabianchi pamoja na eneo la Watu wenye Ulemavu;

ix. Kuratibu na Kushiriki mikutano mbalimbali baina ya SMZ, SJMT na wadau;

x. Kuratibu shughuli za ufuatiliaji na tathmini juu ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kazi za kawaida;

xi. Kufanya tathmini na mapitio ya Mpango Mkakati wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wa mwaka 2021/2022 -2025/2026; na

xii. Kujenga uwezo kwa watumishi na kuweka mazingira bora ya kufanyia kazi.

xiii. Kuratibu ukamilishaji wa sera ya Taifa ya UKIMWI, sera ya Mazingira na kanuni ya taka za kielektroniki.

**Programu ndogo S0403: Uratibu wa Afisi Kuu – Pemba**

97. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu ndogo ya Uratibu wa Afisi Kuu – Pemba inaombewa jumla ya **TZS. 1,434,105,000**. Kati ya fedha hizo, **TZS. 764,970,000** ni kwa ajili ya mshahara na T**ZS. 500,015,000** ni kwa ajili ya

matumizi mengineyo na ruzuku ya **TZS. 169,120,000** kwa Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu.

98. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga shabaha zifuatazo:-

i. Kuratibu ziara za Viongozi Wakuu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza pamoja na shughuli zinazotekelezwa na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba;
ii. Kuratibu mafunzo kwa watumishi wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Pemba;
iii. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji;
iv. Kufanya matengenezo madogo madogo ya jengo la Afisi;
v. Kuratibu vikao 4 vya wadau katika maswala mtambuka;
vi. Kuratibu matayarisho ya mipango na bajeti ya Afisi;na
vii. Kuratibu ufuatiliaji na tathmini wa shughuli za kawaida na miradi ya Afisi ya Makamu Wa Kwanza wa Rais Pemba kwa kila robo mwaka.

## PROGRAMU KUU P03: URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS.

99. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha wa 2026/2027 Programu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Kwanza Wa Rais inaombewa jumla ya TZS 1,622,009,000 kati ya fedha hizo, TZS 772,009,000

ni kwa ajili ya mishahara na TZS. 850,000,000 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

100. **Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii ndogo, Afisi imepanga kutekeleza shabaha zifuatazo:-

i. Kuratibu safari za kikazi za ndani na nje ya nchi;
ii. Kuimarisha huduma za usafiri na mawasiliano;
iii. Kuimarisha huduma za wafanyakazi;
iv. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa Afisi;
v. Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wafanyakazi;
vi. Kufanya matengenezo madogo madogo yanayojumuisha ujenzi wa hodhi la maji, ujenzi wa kibanda cha mlinzi na uwekeji wa bustani katika nyumba ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Kwanza wa Rais; na
vii. Kutatua changamoto za kijamii.
viii. Kutoa misaada kwa vikundi na wananchi mbali mbali wenye mahitaji.

**PROGRAMU KUU P02: USIMAMIZI WA MAZINGIRA**

101. **Mheshimiwa Spika,** Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais inakusanya mapato kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira. Kwa mwaka 2026/2027 imepangiwa kukusanya mapato ya **TZS. 854,019,000** ambazo zinatokana na ada ya uhifadhi na ada ya ukaguzi wa mazingira kwa ajili ya kuchangia mapato ya Serikali.

100. **Mheshimiwa Spika,** Fungu 034 ili liweze kutekeleza majukumu yake naiomba Kamati yako

kuidhinisha **TZS. 4,931,467,000**. Kati ya fedha hizo, **TZS. 1,150,820,000** ni kwa ajili ya mishahara , **TZS. 1,168,668,000** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, na kwa ajili ya miradi ya maendeleo **TZS. 2,611,977,000** ambapo **TZS.2,500,000,000** kutoka SMZ na **TZS. 111,977,000** kutoka kwa washirika wa maendeleo.

**102. Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2026/2027, Afisi kupitia programu hizi imejipangia kutekeleza shabaha zifuatazo: -

i. Kutekeleza Programu ya kurithisha Zanzibar ya Kijani;

ii. Mradi wa kuanzisha mifumo ya kidigitali ya Mazingira;

iii. Kufanya Ufuatiliaji wa maeneo 240 ya Kimazingira Unguja na Pemba;

iv. Kufanya ufuatiliaji wa miradi 240 ya kiuchumi Unguja na Pemba;

v. Kuratibu Tathmini 240 za Athari za Kimazingira na Kijamii;

vi. Kuelimisha jamii juu ya uhifadhi wa mazingira;

vii. Kuandaa Mpango Mkakati wa miaka mitano wa ZEMA;

viii. Kufanya Tathmini na upembuzi yakinifu kwa kupitia na kuangalia vyanzo vipya vya mapato;

ix. Kufanya operesheni 180 za kusimamia upigaji marufuku mifuko ya plastiki Unguja na Pemba;

x. Kufanya operesheni 180 za Kusimamia Maliasili zisizorejesheka Unguja na Pemba;
xi. Kuandaa na Kusimamia Vikao vya Bodi ya ZEMA;
xii. Kuandaa Vikao vya Mashirikiano kati ya ZEMA na Afisi ya Makamu wa Rais Muungano na NEMC;
xiii. Kuandaa maandiko ya miradi na
xiv. Kushiriki matukio ya kitaifa na kimataifa
xv. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa shughuli za Afisi

**PROGRAMU KUU P01: UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA**

**103. Mheshimiwa Spika,** fungu 032 ili iweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naliomba Baraza lako iidhinishe jumla ya **TZS. 13,274,460,000** ambapo **TZS. 2,386,300,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 2,638,160,000** kwa ajili ya matumizi ya mengineyo na T**ZS. 8,250,000,000** kwa ajili ya kutekeleza kazi za maendeleo kupitia fedha za SMZ.

**104. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii, Afisi imepanga kutekeleza yafuatayo: -

1. Kufanya Operesheni 4 kubwa na za kawaida 24 za dawa za kulevya Unguja na Pemba;
2. Kuhakiki na kuteketeza vielelezo vya dawa za kulevya;
3. Kufanya vikao 2 vya wadau wa sheria;

4. Kufanya mikutano 4 ya Tiba za kifamilia;
5. Kujenga kituo cha Tiba na marekebisho ya Tabia Pemba;
6. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa shughuli za Afisi;
7. Kufanya utafiti unaohusu matumizi ya Dawa za kulevya;
8. Kukusanya taarifa za kiintelijensia, kufanya uchunguzi na kufuatilia kesi za dawa za kulevya Mahkamani;
9. Kujenga uelewa wa jamii juu ya athari za dawa za kulevya;
10. Kuendeleza huduma za Tiba na Marekebisho ya Tabia;
11. Kuanzisha na kuendeleza klabu za skuli za kupiga vita dawa za kulevya na
12. Kuendesha vikao vya Baraza la Taifa la kudhibiti na kupambana na dawa za Kulevya
13. Kuandaa na kushiriki matukio ya kitaifa

## PROGRAMU KUU P02: URATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI

**105. Mheshimiwa Spika,** fungu 033 ili Liweze kutekeleza Programu zake kwa ufanisi kwa mwaka wa fedha 2026/2027, naiyomba Kamati yako iidhinishe jumla ya **TZS 2,682,479,602** ambapo **TZS.826,277,000** kwa ajili ya mishahara, **TZS. 1,856,202,602** kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**106. Mheshimiwa Spika,** kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kupitia programu hii, Afisi imepanga kutekeleza shabaha zifuatazo:-

i. Kufanya uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI;
ii. Kutoa elimu kamili na sahihi juu ya maambukizi ya VVU na UKIMWI na mimba za umri mdogo kupitia makundi mbalimbali ya vijana;
iii. Kuhamasisha matumizi ya huduma za VVU na UKIMWI ikiwemo kondomu, ARV, kuhudhuria kliniki na kupinga unyanyapaa;
iv. Kufanya mapitio ya sheria ya kukinga na kusimamia masuala ya UKIMWI na kusimamia utekelezaji wa miongozo ya kitaifa ya UKIMWI;
v. Kuandaa na kushiriki matukio ya kitaifa
vi. Kufanya uhamasishaji wa upatikanaji wa rasilimali za ndani ili kuwa na muitiko endelevu na kupunguza utegemezi;
vii. Kufanya uhamasishaji kwa sekta za utalii kuzingatia masuala ya UKIMWI;

viii. Kuandaa mfumo wa usajili na utambuzi wa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI na wadau;
ix. Kuandaa na kushiriki Vikao vya Mashirikiano kati ya SJMT na SMZ;na
x. Kutoa huduma za utawala na uendeshaji wa Afisi.

## F.SHUKURANI

**107. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kutoa maelezo hayo, natumia fursa hii tena kumshukuru Mwenyezi Mungu

kwa kuniwezesha kuwasilisha hotuba hii mbele ya Kamati yako. Aidha, Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais, inatanguliza shukurani zake za dhati kwa mashirikiano mazuri kupitia Taasisi mbali mbali zinazofanya kazi kwa pamoja zikiwemo Taasisis za Seriakali, Taasisi binafsi, Washirika wa Maendeleo, Taasisi za kifedha, Asasi za kiraia pamoja Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Jamii kwa ujumla na wote waliochangia kwa namna moja au nyengine kufanikisha utendaji wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Miongoni mwa Taasisi za kiserikali zikiwemo, Afisi ya Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Afisi ya Waziri Mkuu, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Wizara ya Fedha na Mipango, Afisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalumu za SMZ, Afisi ya Rais Kazi Uchumi na Uwezekazaji, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Wizara ya Kilimo Umwagiliaji Maliasili na Mifugo, Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Wizara ya Mawasiliano Ujenzi na Uchukuzi, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, Wizara ya Maji Nishati na Madini, Wizara ya Vijana na Uwezeshaji, Wizara ya Ardhi Maendeleo ya Makaazi, Wizara ya Afya na Afisi ya Mwanasheria Mkuu. Vile vile, tunazishukuru Taasisi na Mashirika zikiwemo Baraza la Taifa la Usimamizi na Uhifadhi wa Mazingira (NEMC), Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya Tanzania,ZPDB, ZBA, ZFDA, ZARI, Mkemia Mkuu, DPP, Mahakama,

Tume ya Sayansi na Teknolojia Tanzania (COSTECH), UNDP, World Bank, UNEP, GEF, GCF, UNODC, UK-Border Force, British Kingdom, UNFPA, UNICEF, Global Fund, PEPFAR, UNAIDS, Qatar Charity, DEA, Madrasa Earlier Childhood Program, NAD, NOAH, Emarates Lessure, Muzdalifah foundation na Climate Action Network Tanzania. Pia, nazishukuru taasisi zote zisizo za kiserikali zikiwemo ANGOZA, ZACCA, ZAPHA+, PIRO, ZMBF, MIFF, ZAYEDESA, ZANPUD, ZYF, AATF, ARC, TFED, TULIVE Private Equity Limited na Safari solution kwa kufanya kazi na Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais na ninawashukuru sana Viongozi wa Dini katika kutusaidia kujenga imani za waumini katika kupambana na dawa za kulevya, maambukizo ya ukimwi, uhifadhi wa mazingira na kuwajali Watu wenye Ulemavu.

**108. Mheshimiwa Spika,** Naomba nimshukuru kwa dhati Katibu Mkuu Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Bi Maryam Juma Abdalla kwa namna anavyonisaidia katika kutekeleza majukumu yangu. Pia nawashukuru Wakuu wa Taasisi na Idara zote za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais wakiwemo Wakurugenzi, Makamishna na wenye viti na wajumbe wote wa Bodi zinazosimamia Taasisi za Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa utendaji wao makini. Aidha, kwa upekee ninawashukuru watumishi na watendaji wote wa Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu. Nikiri kuwa, mashirikiano hayo yamekuwa


yakirahisisha sana na kunipa moyo katika kufanya kazi za utekelezaji wa majukumu tuliyopangiwa kwa urahisi na ufanisi mkubwa.

109. **Mheshimiwa Spika,** Mwisho, kwa namna ya kipekee natanguliza shukurani zangu za dhati kwa Wakala wa Uchapaji wa Serikali Zanzibar na vyombo vya habari vya Serikali na binafsi kwa kuiunganisha vizuri sana Afisi yetu na jamii. Michango yao imesaidia sana katika kurahisisha utekelezaji wa majukumu yetu ya kila siku.

## HITIMISHO

110. **Mheshimiwa Spika,** Nawaomba wajumbe wa Baraza lako tukufu waichangie hotuba hii, watushauri ipasavyo na hatimae waidhinishie Afisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais makusanyo ya mapato **TZS. 854,019,000** na fedha za matumizi ya **TZS .35,558,539,602** ili kutekeleza kazi za kawaida na kazi za maendeleo kwa mwaka wa fedha 2026/2027 kwa mchanganuo uliotolewa.

**Mheshimiwa Spika**, Naomba kuwasilisha.



**HAMZA HASSAN JUMA (MBM)**
**KAIMU WAZIRI WA NCHI, AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS,**
**ZANZIBAR.**

## KIAMBATANISHO NAMBARI 1: Muhutasari wa Makusanyo ya Mapato kwa kipindi cha Julai 2025-Machi 2026


| Aina ya Mapato | Kilichopangwa kwa mwaka (2025/2026) | | Jumla | Kilichopangwa kwa miezi tisa (Julai 2025 - Machi 2026) | | Jumla | Kilichokusanywa kwa miezi tisa (Julai 2025 - Machi 2026) | | Jumla | % ya Mwaka (2025/2026) | % ya miezi tisa (Julai 2025 - Machi 2026) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Unguja | Pemba | | Unguja | Pemba | | Unguja | Pemba | | | |
| Uhifadhi wa Mazingira | 346,500,000 | 118,301,000 | **464,801,000** | 265,200,000 | 86,900,000 | **352,100,000** | 248,700,000 | 68,540,000 | **317,240,000** | 68 | 90 |
| Ukaguzi wa Mazingira | 188,000,000 | 48,000,000 | **236,000,000** | 136,000,000 | 41,000,000 | **177,000,000** | 72,200,000 | 0.0 | **72,200,000** | 31 | 41 |
| **Jumla** | **534,500,000** | **166,301,000** | **700,801,000** | **401,200,000** | **127,900,000** | **529,100,000** | **320,900,000** | **68,540,000** | **389,440,000.0** | **56** | **74** |


# KIAMBATANISHO NAMBARI 2: Muhutasari wa Upatikanaji wa Fedha Julai 2025 - Machi 2026


| PROG RAMU | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO MIEZI 9 (JULAI 2025-MACHI 2026) | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | DEVO | JUMLA | MISHAHARA | %YA MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | % YA OC | RUZUKU | % YA RUZUKU | DEVO | JUMLA | % JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PB0101: Uratibu wa Mabadiliko ya Tabia ya nchi | 6,837,611,000 | 6,468,031,503 | 315,964,597 | 402,758,361 | | 5,749,308,545 | 6,468,031,503 | 283,517,062.50 | 90 | 66,608,353 | 17 | | | 880,130,700 | 1,230,256,116 | 19 |
| PB0102: Usimamizi wa Masuala ya Watu Wenye Ulemavu | 1,944,100,000 | 1,563,990,000 | - | - | 1,563,990,000 | - | 1,563,990,000 | | - | | | 761,939,244 | 49 | | 761,939,244 | 49 |
| SB010301: Uongozi wa Rasilimali watu na Uendeshaji | 1,534,843,291 | 1,127,864,473 | 594,322,945 | 533,541,528 | - | - | 1,127,864,473 | 655,430,792.50 | 110 | 256,568,030 | 48 | | | | 911,998,823 | 81 |
| SB010302: Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 355,559,531 | 281,335,713 | 139,447,715 | 141,887,998 | - | - | 281,335,713 | 125,321,575 | 90 | 49,897,811 | 35 | | | | 175,219,386 | 62 |
| SB010303: Uratibu na utekelezaji wa shughuli za OMKR Pemba | 1,065,286,178 | 820,227,088 | 506,957,970 | 313,269,119 | - | - | 820,227,088 | 513,834,000 | 101 | 200,093,079 | 64 | | | | 713,927,079 | 87 |
| PB103: Programu kuu ya Uendeshaji na Uratibu wa Afisi ya Makamu wa Kwanza Wa Rais | 2,955,689,000 | 2,229,427,275 | 1,240,728,630 | 988,698,645 | | | 2,229,427,275 | 1,294,586,367 | | 506,558,920 | | | | | | |
| PB0104: Uratibu wa shughuli za Makamu wa Kwanza wa Rais | 1,239,836,000 | 931,377,131 | 564,531,773 | 366,845,358 | - | | 931,377,131 | 490,709,197.50 | 87 | 89,497,306 | 24 | | | | 580,206,504 | 62 |
| **Jumla 002** | **12,977236,000** | **11,192,825,909** | **2,121,225,000** | **1,758,302,364** | **1,563,990,000** | **5,749,308,545** | **11,192,825,909** | **2,068,812,628** | **98** | **662,664,579** | **38** | **761,939,244** | **49** | **880,130,700** | **4,373,547,150** | **39** |


| PROG RAMU | BAJETI YA MWAKA 2025/2026 | MAKADIRIO MIEZI 9 (JULAI 2025- MACHI 2026) | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU | DEVO | JUMLA | MISHAHARA | %YA MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | % YA OC | RUZUKU | % YA RUZUKU | DEVO | JUMLA | % JUMLA |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| PB0401 na PB0402: Usimamizi wa Mazingira (B04) | 3,085,100,000 | 2,429,676,000 | 897,075,000 | 623,426,000 | - | 909,175,000 | 2,429,676,000 | 929,989,520 | 104 | 260,564,134 | 42 | | | 45,967,155 | 1,236,520,809 | 51 |
| PC0401 na PC0402: Udhibiti wa Dawa za Kulevya (C04) | 8,740,600,000 | 7,744,469,000 | 1,600,350,000 | 1,644,119,000 | - | 4,500,000,000 | 7,744,469,000 | 1,553,631,155 | 97 | 880,337,000 | 54 | | | | 2,433,968,155 | 31 |
| PC0501 na PC0502: Uratibu wa muitiko wa Taifa wa UKIMWI (C05) | 2,379,172,000 | 1,827,727,784 | 722,001,284 | 537,641,250 | - | 568,075,250 | 1,827,717,784 | 603,144,662 | 84 | 244,695,407 | 46 | | | 391,224,960 | 1,239,065,029 | 68 |
| **JUMLA NDOGO** | **14,204,8762,000** | **12,001,872,784** | **3,219,426,284** | **2,805,186,250** | **0** | **568,075,250** | **12,001,862,784** | **3,086,765,337** | **96** | **1,385,596,541** | **49** | **0** | **0** | **437,192,115** | **4,909,553,993** | **41** |
| **JUMLA KUU** | **27,182,108,000** | **23,194,698,693** | **5,340,651,284** | **4,563,488,614** | **1,563,990,000** | **11,726,558,795** | **23,194,688,693** | **5,155,577,964** | **97** | **2,048,261,120** | **45** | **761,939,244** | **49** | **1,317,322,815** | **9,283,101,143** | **40** |


**KIAMBATANISHO NAMBARI 3: Mafanikio**





THAMANI YA MALI ZILIZOTAIFISHWA
1.2E+09
1E+09
800000000
600000000
400000000
200000000
0
2024/2025
2025/2026


IDADI YA KESI ZILIZOFUNGULIWA
120,000,000
100,000,000
80,000,000
60,000,000
40,000,000
20,000,000
0
2024/2025
2025/2026


KIWANGO CHA FEDHA ZA MIKOPO KILICHOTOLEWA TZS.
120,000,000
100,000,000
80,000,000
60,000,000
40,000,000
20,000,000
0
2024/2025
2025/2026


IDADI YA VIFAA SAIDIZI VILIVYOTOLEWA NA VYA UJASIRIAMALI VILIVYOTOLEWA.
900
800
700
600
500
400
300
200
100
0
2024/2025
2025/2026

# KIAMBATANISHO NAMBARI 4: Idadi ya vifaa saidizi vilivyogaiwa.


| NAM | TAASISI | AINA YA KISAIDIZI | IDADI | W/WAKE | W/UME | UNGUJA | PEMBA | THAMANI YAKE |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Qatar Charity | Mashine za kusagia nafaka | 5 | | 5 | 5 | | 60,000,000 |
| 2 | Qatar Charity | Motor Wheelchair | 60 | 26 | 36 | 45 | 15 | 450,000,000 |
| 3 | Baraza la Taifa la Watu wenye Ulemavu All about Albinism | Sun Screen Lotion for Albino | 377 | 162 | 215 | 177 | 200 | 22,620,000 |
| | | Kofia | 236 | 96 | 140 | 106 | 130 | 3,452,000 |
| | | Miwani | 100 | 40 | 60 | 50 | 50 | 1,000,000 |
| | | **Jumla** | **773** | | | | | **27,072,000** |

**KIAMBATANISHO NAMBARI 5: Orodha ya majengo ya umma yaliyokaguliwa**


| SN | WIZARA | MRADI | HALI HALISI | MAHALA ULIPO |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Wizara ya Afya | Nyumba za wafanyakazi wa hospitali ya wilaya-Kinyasini | Majengo yote yamezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kiwango cha wastani | Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Micheweni, Kinyasini Pemba |
| | | Kituo cha afya Jadida | | Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Wete, Jadida Pemba |
| | | Kituo cha Afya Konde | | Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Micheweni, Konde Pemba |
| | | Kituo cha Afya Maziwa Ng'ombe | | Mkoa wa Kaskazini, Wilaya ya Micheweni, Maziwa Ng'ombe Pemba |
| 2 | Wizara ya Ofisi ya Rais Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma, | Mahkama ya Konde | Jengo lote limezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kiwango cha wastani | Mkoa wa Kaskazi, Wilaya ya Micheweni, Konde Pemba |
| 3. | Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni, Sanaa na Michezo | ZBC Radio na Televisheni | Majengo yote yamezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kiwango cha wastani. | Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chakechake Pemba. (Mkoroshoni) |
| | | Uwanja wa Mpira Gombani | | Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chakechake Pemba. (Gombani) |
| | | Jengo la Wizara ya Habari | | Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chakechake Pemba. (Gombani). |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 4. | Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali | Mradi Jengo la Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Pemba | Jengo lote limezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kiwango cha wastani. | Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chakechake Pemba. (Uwanja Tennis). |
| 5. | Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda | Karafu house (ZSTC) | Jengo lote limezingatia mahitaji ya watu wenye ulemavu kwa kiwango cha wastani. | Mkoa wa Kusini, Wilaya ya Chakechake Pemba. (Madungu). |


**KIAMBATANISHO NAMBARI 6: Maeneo ya Kimazingira yaliyofuatiliwa Kiwilaya**




**KIAMBATANISHO NAMBARI 7: Miradi ya Kiuchumi na Kimaendeleo iliyofanyiwa Ufuatiliaji wa Kimazingira**



**KIAMBATANISHO NAMBARI 8: Miradi iliyofanyiwa Tathmini za Kimazingira**



**Kiambatisho nambari 9**: **Idadi ya vijana waliofikiwa kupitia mitandao ya kijamii**

| **Jukwaa** | **Jumla waliofuatilia** | **Wafuatiliaji wapya** | **Jumla walioangalia** | **Walioshiriki** | **Jumla waliofikiwa** |
|---|---|---|---|---|---|
| Instagram | 3,391 | 142 | 109,336 | 304 | 52,057 |
| Facebook | 1,222 | 13 | 83,336 | 207 | 38,057 |
| TikTok | 38 | 9 | 2,007 | - | - |
| **Jumla** | **4,651** | **164** | **194,679** | **511** | **90,114** |

**Kiambatanisho nambari 10A**: **Idadi ya Vijana waliopata huduma na elimu kupitia vituo vya huduma Rafiki na huduma masafa.**

| Aina ya huduma | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|
| Elimu ya VVU na afya ya uzazi | 6,650 | 3,782 | 9,026 |
| Uchunguzi wa magonjwa ya kujamiiana | 2,357 | 1,050 | 3,407 |
| Uzazi wa Mpango | 1,202 | -- | 1,202 |
| Vielelezo vya elimu | ---- | ---- | 1,330 |
| Kondom | ----- | -------- | 2,594 |
| | | | |

**Kiambatanisho nambari 10B**: **Idadi ya watu waliopata huduma na elimu kupitia kliniki za tiba.**

| Aina ya huduma | Wanawake | Wanaume | Jumla |
|---|---|---|---|
| Kupima VVU | 5,144 | 4487 | 9,561 |
| Uchunguzi wa magonjwa ya kujamiiana | 2,588 | 930 | 3,518 |
| Uzazi wa Mpango | 908 | -- | 908 |
| Uchunguzi wa Saratani | 1,001- | ---- | 1,001 |
| Kondom | ----- | -------- | 230,859 |

Kiambatanisho nambari 11: Utekelezaji wa miradi ya maendeleo

**Jina la mradi:** Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani ya Zanzibar.

**Muda: Miaka mitatu (**2022 hadi 2026)

**Mfadhili: Adaptation Fund**

**Malengo:** Kujenga uwezo wa wakulima wadogo kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa njia za vitendo na ubunifu ambazo zitakuwa na matokeo yenye tija.

| S/N | SHUGHULI ILIYOPANGWA | Utekelezaji | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| **1.** | Ujenzi wa matuta kwa eneo la Bumbwini Mafufuni na Kiongwe kidogo. | Hatua za awali za ujenzi zimeanza ambapo hadi sasa tayari Ziara ya kulikagua eneo la ujenzi imefanyika pamoja na kuandaa Hadidu rejea ya utekelezaji wa kazi hiyo | |
| **2.** | Ujenzi wa kisima na makinga maji eneo la Tovuni, Pemba | Eneo lenye ukubwa wa hekta 24 limejengwa makinga maji | Jumla ya wakulima 271 wanatarajiwa kunufaika na uwepo wa makinga maji hayo |

**Jina la Mradi:** Mradi wa Kuwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi

**Muda:** Miaka 5 (2025 hadi 2030)

**Mfadhili:** WORLD BANK

**Lengo:** Kuimarisha mifumo ya serikali za kitaifa na serikali za mitaa kwa kuwawezesha wanajamii kuweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yao.

| S/N | SHUGHULI ILIYOPANGWA | Utekelezaji | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Kuandaa miongozo na vitini vya kutoa elimu ya Mabadiliko ya Tabianchi kwa Serikali za Mitaa | Nyaraka zote muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa programu ya SCALE zimeandaliwa ikijumuisha Kitini cha kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi kwa Serikali za mitaa kimeandaliwa | |
| 2. | Mikutano ya Kuwajengea uwezo serikali za mitaa na wanajamii juu ya uhimili wa athari za tabianchi katika maeneo yao | Mkutano mmoja wa kujenga uwezo umefanyika ambapo jumla ya Mamlaka ya Serikali za mitaa 11 zilishiriki | Jumla ya Halmashauri/ Baraza ya Miji 11 ya Zanzibar yalipitiwa na kufikia vigezo vya kupata fedha za Tuanze Grant. |
| 3. | Kuandaa mfumo wa kuripoti taarifa za athari ya mabadiliko ya tabianchi katika maeneo mbalimbali Unguja na Pemba | Hatua za awali za matayarisho wa mfumo zimeanza kufanyika ambapo jumla ya kompyuta nne zimenunuliwa, mafunzo ya mfumo wa NAV system kwa ajili ya watendaji yamefanyika | Mafunzo hayo yamejumuisha maofisa mipango, wahasibu na wasimamizi wa mradi |
| 4. | Kuwezesha ushiriki wa Mratibu wa SCALE wa AMKR na wafanyakazi wengine husika katika vikao vya kubadilishana maarifa kuhusu masuala ya mipango na mabadiliko ya tabianchi. | Jumla ya mikutano minne imefanyika ikijumuisha watendaji 13 kutoka maeneo mbalimbali ya Tanzania | Mikutano hiyo ilifanyika Arusha, Morogoro, Dar-es-salam na Zanzibar ikijumuisha Watendaji watano wameshiriki katika mkutano uliofanyika Arusha, Watendaji wawili Morogoro na watendaji wawili Dar-es-salam |

| | | | |
|---|---|---|---|
| **5.** | Kuhudhuria mikutano na mafunzo kwa vitendo | Jumla ya mikutano miwili imefanyika kati ya mikutano minne iliyopangwa kwa ajili ya kufanya tathmini ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizokidhi Masharti ya kupatiwa fedha za kutekeleza miradi ya mabadiliko ya tabianchi kupitia mikutano hiyo | Kikao cha Kwanza cha Kamati ya Uongozi ya Mradi kwa ajili ya Tathmini hiyo imebaini kuwa Mamlaka zote zimekidhi vigezo na masharti ya kupata fedha. |
| **6.** | Kuwezesha ushiriki wa Mratibu wa SCALE wa ZEMA na wafanyakazi wengine husika katika vikao vya kubadilishana maarifa kuhusu masuala ya mipango na mabadiliko ya tabianchi. | Jumla ya watendaji watatu wameshiriki katika vikao hivyo | |

**Jina la Mradi:** Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani

**Muda:** Miaka mitano ( 2022 -2027)

**Mfadhili:** SMZ

**Lengo**: kuhamasisha na kuwawezesha wananchi wote wa Zanzibar na wadau mbali mbali kuelewa umuhimu wa misitu, kuhifadhi miti iliyopo, kupanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae.

| S/N | SHUGHULI ILIYOPANGWA | Utekelezaji | MAELEZO |
|---|---|---|---|
| 1. | Kufanya mikutano ya uhamasishaji katika ngazi mbalimbali | Jumla ya mikutano 8 imefanyika kati ya mikutano 15 iliyopangwa kufanyika | Mikutano hiyo ilihusisha taasisi mbalimbali ikiwemo Wizara ya Afya (upandaji miti katika vituo vya afya), Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali (upandaji miti katika skuli), Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi (upandaji miti kando ya barabara), pamoja na wadau kama NGO ya Maisha Bora, CAN, Community Forestry (Pemba), Chuini Cooperative Society na Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi Tanzania. |
| 2. | Kutayarisha mfumo wa kielektroniki wa usajili wa wadau | Mfumo huo wa usajili umetayarishwa na uko tayari kwa ajili ya matumizi | |
| 3. | Kupanda miti ya aina mbali mbali ikiwemo | Miti hiyo ni pamoja na mikoko 1,000, mikarafuu 300, na miti ya | Miti ilipandwa Unguja na Pemba kwa mashirikiano na wadau mbali mbali. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Kupanda miti ya aina mbali mbali ikiwemo ya matunda na misitu | Miti hiyo ni pamoja na mikoko 1,000, mikarafuu 300, na miti ya matunda mchanganyiko 100, na mikoko 3,000. | Miti ilipandwa Unguja na Pemba kwa mashirikiano na wadau mbali mbali. |
| 4. | Kubaini na kupanda mikoko na miti katika maeneo ya jamii | Jumla ya maeneo 19 yalipandwa miti ya aina mbalimnbali ikiwemo eneo la skuli ya mikindani lilopandwa jumla ya miti 100 kati ya maeneo 5 yaliyopangwa | |
| 5. | Kuanzisha Kitengo cha Usimamizi wa Mradi (PMU) | Kuteuliwa kwa watendaji wa kitengo na kuanza kutekeleza majukumu yao | |

**Kiambatanisho nambari 12: Makadirio ya mapato kwa Mwaka 2026/2027**

| Kasma (034) | Aina ya Mapato | Mkadirio | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Unguja | Pemba | Jumla |
| 1422018 | Uhifadhi wa Mazingira | 455,600,000.0 | 118,420,000.0 | 574,020,000.0 |
| 1422019 | Ukaguzi wa Mazingira | 232,000,000.0 | 48,000,000.0 | 280,000,000.0 |
| | Jumla | 687,600,000.0 | 166,420,000.0 | 854,020,000.0 |

## MWELEKEO WA BAJETI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

| KIFUNGU | PROGRAMU | MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU PE | RUZUKU OC | KAZI ZA MAENDELEO | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | SMZ | WAHISANI |
| **P 01** | **URATIBU WA MABADILIKO YA TABIANCHI** | **7,909,527,000** | 432,286,000 | 363,838,000 | | | 5,000,000,000 | 2,113,403,000 |
| **P 02** | **USIMAMIZI WA MASUALA YA WATU WENYE ULEMAVU** | **1,736,920,000** | | | 788,539,000 | 948,381,000 | | |
| **P 04** | **UONGOZI NA UTAWALA** | **3,401,677,000** | | | | | | |
| S 0401 | Uongozi wa Rasilmali Watu na Uendeshaji | 1,594,227,000 | 920,905,000 | 673,322,000 | | | | |
| S 0402 | Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti | 373,345,000 | 200,000,000 | 173,345,000 | | | | |
| S 0403 | Uratibu na Utekelezaji wa shughuli za Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais - Pemba | 1,434,105,000 | 764,970,000 | 500,015,000 | | 169,120,000 | | |
| **P03** | **URATIBU WA SHUGHULI ZA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS** | **1,622,009,000** | 772,009,000 | 850,000,000 | | | | |
| | **JUMLA YA 002** | **14,670,133,000** | **3,090,170,000** | **2,560,520,000** | **788,539,000** | **1,117,501,000** | **5,000,000,000** | **2,113,403,000** |

## MWELEKEO WA BAJETI YA AFISI YA MAKAMU WA KWANZA WA RAIS KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027


| KIFUNGU | PROGRAMU | MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU PE | RUZUKU OC | KAZI ZA MAENDELEO | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | SMZ | WAHISANI |
| **P 02** | **USIMAMIZI WA MAZINGIRA** | **1,263,116,000** | | | | | | |
| S 0202 | Tathmini na Ufuatiliaji wa Kimazingira | 1,184,752,000 | | 72,773,000 | | | 1,000,000,000 | 111,979,000 |
| S 0201 | Uzingatiaji na Utekelezaji wa Sheria | 78,364,000 | | 78,364,000 | | | | |
| **P 01** | **UONGOZI NA UTAWALA** | **3,668,351,000** | | | | | | |
| S 0101 | Kuimarisha Utendaji wa Ofisi | 3,668,351,000 | 1,150,820,000 | 1,017,531,000 | | | 1,500,000,000 | |
| | **JUMLA YA 034** | **4,931,467,000** | **1,150,820,000** | **1,168,668,000** | **-** | **-** | **2,500,000,000** | **111,979,000** |
| **P 01** | **UDHIBITI WA DAWA ZA KULEVYA** | **9,172,577,000** | | **-** | | | | |
| S 0101 | Uchunguzi, Operesheni wa Dawa za Kulevya na Uhalifu unaofanana nao | 462,397,000 | - | 462,397,000 | | | | |
| S 0102 | Kinga, Tiba na Marekebisho ya Tabia | 8,710,180,000 | | 460,180,000 | | | 8,250,000,000 | |
| **P 02** | **UTAWALA NA RASILIMALI WATU** | **4,101,883,000** | | **-** | | | | |
| S 0201 | Utawala na Rasilimali watu | 2,936,568,000 | 1,826,704,000 | 1,109,864,000 | | | | |
| S 0202 | Kudhibiti Dawa za kulevya Pemba | 1,165,315,000 | 559,596,000 | 605,719,000 | | | | |
| | **JUMLA YA 032** | **13,274,460,000** | **2,386,300,000** | **2,638,160,000** | **-** | **-** | **8,250,000,000** | **-** |
| **P 02** | **KURATIBU MUITIKO WA TAIFA WA UKIMWI** | **759,748,621** | | | | | | |
| S 0201 | Kuratibu, Kufuatilia naKutathmini ya | 559,698,621 | - | 559,698,621 | | | | |

| KIFUNGU | PROGRAMU | MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027 | MISHAHARA | MATUMIZI MENGINEYO | RUZUKU PE | RUZUKU OC | KAZI ZA MAENDELEO | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | | | SMZ | WAHISANI |
| | Muitiko wa Taifa wa UKIMWI | | | | | | | |
| S 0202 | Mawasiliano na Utetezi juu ya masuala ya UKIMWI | 200,050,000 | - | 200,050,000 | | | | |
| **P 01** | **UONGOZI NA UTAWALA** | **1,922,730,981** | | | | | | |
| S 0101 | Uratibu na Uendeshaji Pemba | 407,821,715 | 204,095,000 | 203,726,715 | | | | |
| S 0102 | Utawala na Uendeshaji - Unguja | 1,359,950,516 | 622,182,000 | 737,768,516 | | | | |
| S 0103 | Mipango, Sera na Utafiti | 154,958,750 | - | 154,958,750 | | | | |
| | **JUMLA YA 033** | **2,682,479,602** | **826,277,000** | **1,856,202,602** | **-** | **-** | **-** | **-** |
| | **JUMLA YA TAASISI 032+033+034** | **20,888,406,602** | **4,363,397,000** | **5,663,030,602** | **-** | **-** | **10,750,000,000** | **111,979,000** |
| | **JUMLA KUU 002+032+033+034)** | **35,558,539,602** | **7,453,567,000** | **8,223,550,602** | **788,539,000** | **1,117,501,000** | **15,750,000,000** | **2,225,382,000** |

## Kiambatanisho nambari 14: Fedha za Miradi yaMaendeleo

| Jina La Mradi | Chanzo cha Fedha | Iliyopangwa 2025/2026 | Iliyopatikana 2025/2026 | % ya iliyopat ikana | Makadirio kwa mwaka wa fedha 2026/2027 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mradi wa kuimarisha uhimili wa mabadiliko ya tabianchi kwa jamii za pwani ya Zanzibar | ADAPTATION FUND | 815,220,000 | 645,643,200 | 79 | 1,407,837,000 |
| Mradi wa Kuwezesha Serikali za Mitaa kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi | WORLD BANK | 750,315,877 | 280,454,655 | 37 | 663,760,220 |
| Mradi Shirikishi wa Kuhimili Mifumo ya Ikolojia ya Bahari ya Ukanda wa Pwani na Shughuli za Kujipatia Kipato | UNEP | - | - | - | 153,785,000 |
| **Jumla Washirika wa Maendeleo** | | **2,413,196,582** | **1,317,322,815** | **59** | **2,225,382,000** |
| Mradi wa kuanzisha mifumo ya kidigitali ya Mazingira | SMZ | | | | 1,500,000,000 |
| Mradi wa Usimamizi wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi | SMZ | 4,500,000,000 | - | | 5,000,000,000 |
| Programu ya Kuirithisha Zanzibar ya Kijani - SMZ | SMZ | 1,000,000,000 | - | 0 | 1,000,000,000 |
| Ujenzi wa Kituo cha Tiba na Marekebisho ya Tabia- Pemba | SMZ | 4,500,000,000 | - | 0 | 8,250,000,000 |
| **Jumla SMZ** | | **10,000,000,000** | | | **15,750,000,000** |
| **Jumla Kuu** | | **12,413,196,582** | **1,317,322,815** | **11** | **17,975,382,000** |

## Kiambatanisho nambari 15: MGAWANYO WA FEDHA KIPROGRAMU






Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi akimkabidhi mashine ya kusagia nafaka Bi Rahma Kassim Mtawa mwenye Ulemavu macho wakati wa kilele cha Maadhimisho ya Siku ya Watu wenye Ulemavu Duniani yaliyofanyika katika ukumbi Dkt. Ali Mohamed Shein - Tunguu Zanzibar; Tarehe 03/12/2025



KAIMU Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe.Hamza Hassan Juma (kulia) akimkabidhi KAIMU Katibu Tawala Wilaya ya Kaskazini "A", Unguja Bw. Abdul- Majid Dhamir Ramadhani vifaa mbali mbali vya ujasiriamali kwa niaba ya wananchi wa Matemwe, vifaa hivyo vitatumika katika shughuli za ushoni , upakasaji, kusarifu sabuni na manukato wakati wa hafla ya makabidhiano ya vituo vitatu vya mafunzo kupitia mradi "EBBAR" unaotekelezwa Mtemwe ,Unguja; Tarehe 12 /03/2026.



Miongoni mwa dawa za kulevya zinazotumiwa zaidi na vijana, ambazo zimeendelea kuathiri afya, maisha yao ya baadaye, na kupunguza nguvu kazi ya taifa.




Kongamano la elimu ya VVU na UKIMWI kwa wanafunzi wa vyuo vikuu vya Zanzibar, likilenga kuongeza uelewa kuhusu kinga, upimaji wa hiari, matumizi ya huduma za afya na kuondoa unyanyapaa kwa watu wanaoishi na VVU.

Kongamano hilo linaimarisha mchango wa vijana katika mapambano dhidi ya UKIMWI na kujenga jamii yenye afya na uelewa sahihi.



Eneo la Tumbe, Kaskazini Pemba, limeathiriwa kwa kiasi kikubwa na mabadiliko ya tabianchi, ikiwemo uingiaji wa maji ya chumvi, mmonyoko wa fukwe na kuongezeka kwa joto la bahari—hali inayohatarisha makaazi, kilimo, uvuvi na shughuli nyingine za kiuchumi.